Nipashe
Jumatatu Septemba 14, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0580338
The Guardian digital
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




UKURASA 11



## Ilani SAU yabeba mambo 4 muhimu ya kipaumbele

UKURASA 2

# Kampeni za ACT zaitikisa Zanzibar

**MAPYA** yabainishwa ubia wake na CHADEMA uchaguzi mkuu...*Endelea ukurasa 2*





Mgombea urais wa Zanzibar kupitia Chama cha ACT-Wazalendo, Seif Sharrif Hamad, akuhutubia wakati wa uzinduzi wa kampeni za chama hicho katika viwanja vya Kibandamaiti Zanzibar jana. **PICHA: MTANDAO**

## Magufuli, Museveni wasaini mkataba bomba la mafuta

UKURASA 3



Rais Dk. John Magufuli akimlaki mgeni wake Rais wa Uganda, Yoweri Museveni, alipowasili kutia saini waraka wa pamoja kuanza mradi wa ujenzi wa bomba la mafuta kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania) kwenye sherehe fupi iliyofanyika Uwanja wa Ndege wa Chato mkoani Geita jana. **PICHA: IKULU**

## YALIYOMO

**UKURASA WA 3**

**MGOMBEA URAIS NCCR KUUNGANISHA ILANI ZA VYAMA**
MGOMBEA urais wa Jamhuri ya Muungano kupitia Chama cha NCCR-Mageuzi, Yeremia Maganja, amesema akiingia madarakani ataunganisha...

**UKURASA WA 5**

**AFUNGWA MIAKA 30 JELA KUBAKA MTOTO**
MKAZI wa Kijiji cha Bukatika Kata ya Matongo katika Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, Shabani Salimu (25), amehukumiwa na...

**UKURASA WA 5**

**VICHWA VIKUBWA, MGONGO WAZI TATIZO KWA WATOTO**
TAASISI ya Mifupa Muhimbili (MOI), inapokea watoto 700 hadi 1,200 kwa mwaka walio na tatizo la vichwa vikubwa...

## TUME YAREJESHA WAGOMBEA WENGINE

UKURASA 4

**MICHEZO** SVEN: SAFARI UBINGWA SIMBA TUNAIANZA J'PILI UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

Fursa kwa Wagombea! 2020
VOTE

Gazeti la Nipashe linawapongeza wateule wote waliopitishwa na vyama vyao kugombea ubunge katika majimbo mbalimbali nchini
Je ungependa kukishukuru chama chako ?
Je ungependa kutangaza sera zako kwa wapiga kura ?
Nipashe inatoa nafasi kutangaza sera zako kwa gharama nafuu

Nipashe
MWANGA WA JAMII
Wasiliana nasi
Simu: 0686 101335,
Barua pepe: advertise@guardian.co.tz
VOTE



Mgombea urais kwa tiketi ya Chama cha Wananchi (CUF), Prof. Ibrahim Lipumba, akiomba kura katika mkutano wa kampeni uliofanyika jana, mkoani Morogoro. **PICHA: BONIFACE GIDEON**

# Kampeni za ACT zatikisa Zanzibar

**Na Khatib Suleiman,**
ZANZIBAR

UZINDUZI wa kampeni za uchaguzi mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo jana, uliutikisa mji wa Zanzibar, ambapo umati wa wakazi ulijitokeza katika viwanja vya Demokrasia Kibandamaiti.

Uzinduzi huo uliendana na kampeni za kuwanadi wagombea urais wa Zanzibar, uwakilishi, ubunge na udiwani kupitia Chama cha ACT-Wazalendo.

Licha ya jua kali lililokuwa likiwaka, lakini wananchi na wafuasi wa chama hicho walifika mapema majira ya saa nne asubuhi viwanjani hapo, ambapo viongozi wa chama hicho walianza kuzungumza majira ya saa kumi jioni.

Katika viwanja hivyo vilipambwa kwa rangi ya zambarau na nyeupe, huku wasanii mbalimbali wakitumbuiza.

**MEMBE AKOSEKANA**

Wafuasi wa chama hicho walitarajia kumuona mgombea wa urais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Bernard Membe, kuhudhuria mkutano huo, lakini hakuwapo.

Mkutano huo pia ulihudhuriwa na Kiongozi Mkuu wa chama hicho, Zitto Kabwe, huku ikielezwa kuwa kesho chama hicho kitaendelea na mikutano yake ya kampeni Kisiwani Pemba.

**MAALIM SEIF ATAJA VIPAUMBELE**

Akiwahutubia wananchi na wapenzi wa chama hicho, mgombea urais wa Zanzibar, Maalim Seif Sharif Hamad, alisema akipewa ridhaa atahakikisha Zanzibar inakuwa na katiba mpya yenye maamuzi kamili.

Alieleza kuwa pia atahakikisha anaimarisha uchumi na kutafuta vyanzo vipya vya mapato ikiwamo kujenga bandari mpya na uwanja wa ndege wa kisasa.

Maalim Seif aliwataka vijana ambao hawajaoa kujiandaa kuoa na wale ambao wana mke mmoja kujiandaa kuongeza mke kwa sababu akiingia madarakani uchumi utaimarika.

Alieleza kuwa Zanzibar ina utajiri mkubwa na vyanzo vingi vya mapato, lakini bado hakuna ubunifu wa kuvitumia vyanzo hivyo.

"Nikipewa ridhaa na wananchi kuiongoza Zanzibar nitahakikisha tunakuwa na Katiba mpya yenye maamuzi kamili," alisema Maalim Seif.

Aidha, aliendeleza kauli yake ya kuwa hatokubali kunyang'anywa ushindi katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu, na kuwataka wafuasi wa chama hicho kulinda kura zao.

Alieleza kuwa atahakikisha anaboresha sekta ya elimu na kutoa elimu bure hadi chuo kikuu ili nchi iweze kupata wataalamu na kuwa na maendeleo.

Alisema hivi sasa milango ya kwenda ikulu ipo wazi baada ya Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) kumthibitisha kuwa mgombea kutokana na kuwekewa pingamizi, lakini alishinda pingamizi hiyo.

**KAULI ZA ZITTO**

Naye Zitto Kabwe alisema kuwa chama hicho kitakaposhinda katika uchaguzi mkuu kitahikikisha kinaunda akaunti ya pamoja kwa ajili ya mapato ya muungano ili Zanzibar iweze kufaidika na mgao wa Muungano.

Aliwataka Wazanzibari kumchagua Maalim Seif ili kuwaletea maendeleo, na kwamba maendeleo hayo hayawezi kupatikana bila ya kuwa na serikali tatu.

Alisema ACT itahakikisha inasimamia Katiba mpya ili Zanzibar iweze kunufaika na maendeleo.

Alieleza kuwa watahakikisha kuwa wagombea wao walioenguliwa na tume ya uchaguzi wanarejeshwa na watafanya maandamano kisiwani Pemba kesho.

# ACT-Wazalendo ipo tayari ubia na CHADEMA

**Na Mwandishi Wetu**

KIONGOZI Mkuu wa Chama cha ACT- Wazalendo, Zitto Kabwe, amesema chama chake kipo tayari kushirikiana na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kuungana mkono kwa wagombea wanaokubalika kwenye majimbo ili waweze kuibuka na ushindi.

Alitoa ufafanuzi huo baada ya ombi la mgombea urais wa CHADEMA, Tundu Lissu, kuachiwa upande wa Tanzania Bara kwa kuwa ndiyo chama chenye misuli ya kushindana na Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Akizungumza na wahariri na waandishi waandamizi wa vyombo mbalimbali vya habari nyumbani kwake jijini Dar es Salaam Alhamisi iliyopita, Lissu alisema kuwa tayari chama hicho kimeshakubali kumwachia mgombea urais wa ACT-Wazalendo, visiwani Zanzibar, Maalim Seif Sharif Hamad.

Zitto aliiambia Nipashe wakati akitoa msimamo wa chama hicho kuwa: "Tunaendelea kuzungumza na CHADEMA kuhusu kushirikiana. Ninaamini kuwa tutakubaliana majimbo ya kuachiana na pia mgombea mmoja wa upinzania wa urais wa kupigiwa kura na wananchi."

Kwa upadne wake Lissu alisema CHADEMA tayari imeshatangaza hadharani kuwa kitamuunga mkono mgombea urais wa Zanzibar wa ACT-Wazalendo, kwa kuwa ndiye anayekubalika na anaweza kumshinda mgombea wa CCM.

Kutokana na hali hiyo, Lissu alisema kwa haraka kwa upande wa Bara chama na mgombea anayeweza kuishinda CCM ni yeye (Lissu) na kukiomba ACT-Wazalendo kufikiria suala hilo na kukubali kumuunga mkono.

"Mazungumzo na ACT-Wazalendo hayajafa ila tumesema Maalim Seif ndiye anaweza kuishinda CCM Zanzibar na ndiyo tutawaunga mkono asilimia 100, sisi tunaweza kuokoteza kura, lakini hatutaweza kuishinda CCM Zanzibar, wagombea wetu tumewataka wamuunge mkono, si msimamo wa Lissu bali uongozi wa CHADEMA," alifafanua.

"Ukiangalia Bara kwa macho angavu anayeweza kuishinda CCM ni CHADEMA, tumependekeza kwa wenzetu watuachie upande wa Bara, hatusemi waachie kila kitu bali yale maeneo ambayo watashinda waendelee, tusigombee kiti kama abiria wa 'Titanic', kikubwa tushinde uchaguzi Bara na Zanzibar halafu tutakaa tuzungumze," alibainisha.

Nipashe ilimtafuta mgombea urais wa ACT- Wazalendo, Bernard Membe, kupata msimamo wake kuhusu suala hilo, simu yake haikupatikana na alivyotumiwa ujumbe mfupi kupitia WhatsApp haukujibiwa.

# Ilani SAU yaja na mambo manne

**Na Yasmine Protace**

CHAMA cha Sauti ya Umma (SAU) jana kilizindua ilani ya uchaguzi pamoja na kampeni katika viwanja vya Kwazoo Kata ya Ukonga jijini Dar es Salaam.

Akizindua ilani hiyo, mgombea urais kupitia chama hicho, Mtamwegwa Mgahywa, alisema kuwa ilani hiyo imejikita katika kuinua kilimo, elimu bure, wajasiriamali kupatiwa mitaji ya kuendelea biashara zao.

"Nimefanya utafiti tangu miaka 30 nikabaini sekta ya kilimo ilivyokuwa na changamoto na hali hiyo inawafanya wakulima kutonufaika na kilimo hicho," alisema.

Aliongeza kuwa akiingia madarakani atahakikisha wakulima wanalima kilimo kwa kutumia trekta na kuachana na kilimo cha mkono.

Alisema atahakikisha wakulima wananufaika na kilimo chao, ambapo mazao watakayouza watayauza kwa bei ya juu.

Kuhusu huduma za afya, ilani yao itawawezesha wajawazito kupata huduma bure na wataacha kwenda na ndoo ikiwamo na vifaa vya kujifungulia.

Akizungumzia wafanyabiashara wadogo wakiwamo mama lishe, baba lishe, atahakikisha wanapatiwa shilingi milioni moja ili waweze kuboresha bidhaa zao.

"Baada ya wafanyabiashara kutufuata sisi kuomba mikopo, sisi tutawafuata wao kuwapatia mikopo," alisema.

Kuhusu elimu, alisema ilani yao itatoa elimu bure kuanzia elimu ya awali hadi chuo kikuu.

Alisema ili kuhakikisha ilani yao inawaletea maendeleo wananchi, wanatakiwa wakichague SAU ili iyatimize yale ambayo wanataka kuwafanyia wananchi.

Alisema chama chao hakipingi maendeleo yanayofanywa na serikali, ila wao watayafanya maendeleo kwa kipindi cha muda mfupi, na maendeleo hayatafanyika kwa kuchukuwa miaka mingi.

## HABARI KITAIFA




Ofisa Usimamizi wa Kodi kutoka Mamlaka ya Mapato (TRA), Zakeo Kowero (kulia), akimwelimisha mfanyabiashara wa stendi kuu katika Manispaa ya Mtwara Mjini ikiwa ni sehemu ya kampeni maalumu ya elimu kwa mlipakodi inayoendeshwa na TRA katika mkoa wa Mtwara ili kuhamasisha ulipaji kodi kwa wakati. **PICHA: NA MPIGA PICHA WETU**

# JPM na Museveni wasaini mkataba bomba la mafuta

**Na Gwamaka Alipipi,** CHATO

SERIKALI za Tanzania na Uganda jana ziliingia makubaliano ya kuanza kwa utekelezaji wa mradi wa bomba la mafuta ghafi kutoka Hoima, Uganda hadi mkoani Tanga, huku Tanzania ikitarajia kuchukua asilimia 60 ya faida itakayopatikana katika mradi huo.

Vilevile, Tanzania inatarajia kunufaika kwa kupata Dola za Marekani milioni 363 (sawa na Sh. trilioni 7.5), zitakazotokana na makusanyo ya kodi kwa kipindi cha miaka 25.

Utiaji saini wa makubaliano ya utekelezaji huo ulifanyika jana mkoani Geita, wilayani Chato kati ya Rais John Magufuli na Rais wa Uganda, Yoweri Museveni.

Akizungumza baada ya mchakato huo, Rais Magufuli alisema mradi huo wenye thamani ya Dola za Marekani bilioni 3.5 (Sh.tilioni 7.8), Tanzania itapata faida mbalimbali ikiwamo kutengeneza ajira za moja kwa moja 10,000 hadi 15,000, kuvutia wawekezaji, kukuza ushirikiano wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Pia kukuza ushoroba wa Kaskazini, zikiwamo nchi za Burundi, Kenya, Rwanda, Sudani Kusini, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), pamoja na kuchochea shughuli za kiuchumi.

"Mradi huu utaleta faida nyingi sana, ni bomba refu zaidi duniani likiwa na urefu wa kilometa 1,415 na teknolojia ya kisasa ya kusafirisha mafuta yakiwa na joto. Kilometa 330 zitakuwa Uganda, kilometa 1,115 zitakuwa Tanzania," alisema Rais Magufuli na kuongeza:

"Kwa upande wa Tanzania bomba hili litapita katika mikoa nane ambayo ni Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara, Tanga, pia litapita katika wilaya 24, kata 132, pamoja na vijiji 186, kote huko litatoa ajira," alisema Rais Magufuli.

Kadhalika, alisema wakazi zaidi ya 90,000 watakaoguswa na utekelezaji wa mradi huo watalipwa fidia ya Sh. bilioni 21 ili kupisha ujenzi.

"Rais Museveni amefanya mambo makubwa yasiyowezekana Afrika Mashariki kwa kugundua mafuta, haya mambo tulikuwa tukiyasikia tu katika nchi za uarabuni...yawezekana mazuri uliyoyafanya ukaambulia matusi, lakini ninachokusihi wewe chapa kazi na uwasamehe," alisema Rais Magufuli.

Matokeo ya mradi huo alisema utawezesha uchumi wa Uganda na Tanzania kukua, pamoja na kuongeza undugu baina ya nchi mbili.

Akizungumzia utekelezaji wa mradi huo, alisema ulikwamishwa na mlipuko wa ugonjwa wa virusi vya corona, na kwamba juzi alipigiwa simu na Rais Museveni akielezwa kukamilika kwa mazungumzo na kuomba makubaliano ya utekelezaji yafanyike.

Rais Magufuli alisema: "Baada ya kupigiwa simu na Rais Museveni na kuomba kuja Tanzania, nikamwambia njoo hata kesho, akaniambia atakuja na barakoa, nikamjibu wewe njoo hata na branketi uje kulala huku huku...Huu ni ushindi wa pili wa kiuchumi kati ya Tanzania na Uganda baada ya ule wa awali wa kumwondoa Iddi Amini."

Naye Rais wa Museveni alisema wataalamu wazawa ndio waliogundua hazina hiyo ya mafuta yapatayo mapipa bilioni 6.1.

"Tulitumia wataalamu wetu kuanzia hatua ya kwanza hadi ya mwisho, watu wa nje (wazungu) walikuwa wanatuchezea. Tulichokifanya tuliwachukua wazawa wetu waliosomea masuala ya Geology (elimu ya miamba), Geo-Physics, Chemistry (kemia) katika vyuo vikuu vya jijini London, Romania, Algeria, ambao wakasomea uzamili wa masuala ya mafuta," alisema Rais Museveni na kuongeza:

"Mwaka 2006 ndiyo tuligundua mafuta hayo, muda mwingi wataalamu wangu walikuwa wanavutana na kampuni za kigeni juu ya kodi tutakayopata," alisema Rais Museveni.

Naye Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG), Prof. Adelardus Kilangi, akitaja makubaliano matatu yaliyomo katika mkataba huo kuwa: Mosi ni kila nchi kuchukua hatua za haraka kati yake na kampuni husika zitakazohusika katika mradi huo.

Pili, kila nchi kukamilisha kwa haraka mashauriano ya mikataba midogo itakayotakiwa kutekelezwa, tatu ni kila nchi kuchukua hatua ili kuwezesha utekelezaji wa haraka wa bomba la hilo la mafuta.

# Mgombea NCCR kuunganisha ilani za vyama

**Na Elizabeth Zaya**

MGOMBEA urais wa Jamhuri ya Muungano kupitia Chama cha NCCR-Mageuzi, Yeremia Maganja, amesema akiingia madarakani ataunganisha ilani za uchaguzi za vyama vyote kupata moja kwa ajili ya kuendesha serikali miaka mitano ijayo.

Akizungumza na Nipashe kuhusu namna chama hicho kilivyojiandaa kwenye kampeni na kitakavyoingia madarakani, Maganja alisema lengo la kuunganisha ni kupata ilani bora ambayo itawaunganisha wote kulingana na matamanio yao.

Alisema katika kuchambua ilani hizo, watatumia wataalamu wabobezi (think tank) katika sekta zote nchini ambao hawafungamani na chama chochote cha siasa ili kuhakikisha kwamba inapatikana moja ambayo ni bora zaidi.

"Sisi tunaamini kwamba kila ilani ya uchaguzi ya kila chama cha siasa ina baadhi ya mambo ambayo ni mazuri, tukiingia madarakani tutakusanya ilani zote na kuzipeleka kwa wataalamu watuchambulie yale mazuri na kupata moja ambayo ndiyo itatumika kuendesha serikali kwa miaka mitano," alisisitiza Maganja.

"Na kwa sababu tumepanga kwamba tukiingia madarakani tutatengeneza Katiba mpya, hilo ni miongoni mwa mambo ambayo tutaliingiza ili chama chochote kinachoingia madarakani kifuate utaratibu huo, na ilani hizo zitakuwa zinakusanywa miezi minne kabla ya uchaguzi na kuchambuliwa na wataalam ili anayekuwa anaingia madarakani aitumie hiyo."

Kwa mujibu wa Maganja, atahakikisha wanapitia upya mchakato uliotumika kuwaondoa wafanyakazi wote kazini kwa madai ya vyeti feki.

Alisema kwamba kama hawakulipwa jasho lao baada ya kufukuzwa, serikali yake itahakikisha inawalipa wote.

"Hawa wafanyakazi walioondolewa kazini, waliajiriwa kihalali na serikali, kwa hiyo kama ni makosa serikali ndiyo ilifanya. Kwa hiyo tukiingia madarakani, tutaanza upya 'ku-review' (kupitia) namna walivyoingia, walivyofanya kazi na namna serikali ilivyotekeleza kazi ya kuwaondoa," alisema Maganja.

"Tunaamini kwamba hata kama walifoji vyeti, lakini serikali iliwaamini na ndiyo iliyowaajiri na wamelitumikia taifa wengine miaka 10, 20, 30, kwa hiyo huwezi kuwaondoa kienyeji hivi, lazima tutaliangalia hili kwa upya na tutalifanyia kazi, na kama kuna haki zao ambazo walistahili kulipwa na hawakufanyiwa hivyo, sisi tutalifanya kwa kushauriwa wa wataalamu ikiwamo Shirika la Kazi Duniani (ILO)."

"Tutaangalia waliingiaje, makosa yao na ya serikali katika kuwaingiza kazini yalikuwa yapi, hawa ni binadamu kwa hiyo lazima tuangalie namna pia walivyotoka ili kuifanya sekta ya umma iwe ya kuheshimika."

Mgombea huyo alisema endapo wataingia madarakani ni watahakikisha kwamba wanafunzi wote waliopata ujauzito na kufukuzwa shule wanarejea masomoni.

"Wanafunzi hawa wataendelea na masomo mpaka pale ambapo wataalamu wa afya watathibitisha kwamba wanahitaji kusimama kwa ajili ya kujifungua na baada ya hapo watarejea shuleni kuendelea na masomo kama kawaida," alisema Maganja.

"Mwanaume na mwanamke wanatakiwa kupewa fursa sawa, tunaamini kwamba suala la wanafunzi kupata ujauzito kunasababishwa na mambo mengi ikiwamo mazingira tuliyonayo ambayo si rafiki pamoja na matatizo mengine, kwa hiyo ili haki itendeke kwa watoto wote wa kike na kiume kupata elimu, hatutamfukuza shule."

Alisema kuendelea kufukuza wanafunzi wa kike wanaopata ujauzito shuleni ni kuendelea kutengeneza taifa tegemezi.

# Washauriwa kumtanguliza Mungu uchaguzi mkuu

**Na Jumbe Ismailly,** IKUNGI

WAUMINI wa madhehebu ya dini mbalimbali nchini wametakiwa kuendelea kumtanguliza Mungu wakati wakijiandaa na uchaguzi mkuu wa rais, wabunge na madiwani unaotarajiwa kufanyika Oktoba 28, mwaka huu.

Askofu Mkuu wa Kanisa la International Evangelism Church, Dk. Eliud Isanjya, alitoa ushauri huo wakati wa ibada ya shukrani ya kutimiza miaka 50 ya utumishi mtakatifu wa Askofu Jacob Nyika iliyofanyika katika kanisa hilo lililopo katika mji mdogo wa Ikungi, mkoani Singida.

Dk. Isanjya aliwataka waumini wa madhehebu yota kutambua umuhimu wa uchaguzi huo.

"Huu ni mwaka wa uchaguzi na kampeni zinaendelea. Hili jambo ni kubwa kwa nchi yetu na tungependa tumwambie Mungu jinsi ambavyo tusingependa tufanye wenyewe, bali yeye ahusike," alisema Dk. Isanjya.

Pia alisema ili uchaguzi huo ufanyike kwa amani, utulivu na upendo ni wakati mwafaka sasa wa kumkaribisha Mungu kuhakikisha ili afanikishe jambo hilo salama.

Kwa mujibu wa Dk. Isanjya, katika kipindi cha miaka mitano ya Rais John Magufuli wameendelea kushuhudia nchi ikiongozwa kwa amani, maendeleo na kwamba wanaamini hali hiyo itaendelea kuwapo.

Kwa upande wake, Askofu Moses Mapunda kutoka Dar es Salaam alimpongeza Askofu Jacobo Nyika kwa utumishi wake uliotukuka.

"Kutokana na hekima na busara alizonazo Askofu Nyika, bado ushauri wake unahitajika katika kazi ya Mungu. Kwa hiyo tunamwomba Mungu ampe maisha marefu katika kumtumikia na kutimiza kusudi lake hapa duniani," alisema Askofu Nyika.

Akizungumza na waumini wa kanisa hilo, Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Rehema Nchimbi, alitumia fursa hiyo kukemea suala la ukabila kwa kuwataka waumini hao kuondokana na dhana hiyo kwa kuwa haikubaliki katika nchi ya Tanzania hususani katika kipindi hiki cha uchaguzi mkuu.

"Suala la ukabila liondoke na ninasema hivi kwa sababu hata katika suala la uchaguzi huu watu wanaenda na ukabila, suala hapa siyo ukabila, hapa ni Mungu aliyehai, na nathubutu kusema kwamba kama kuna mungu wa Elia, Yakobo na Isaka, basi pia ni Mungu wa Magufuli," alisema Dk. Nchimbi.



Mkuu wa Wilaya ya Musoma, Dk. Vincent Anney Naano (wa pili kushoto), akikata utepe kuzindua duka jipya la kisasa la Vodacom lililopo Musoma Mjini juzi. Wengine kushoto ni msimamizi wa duka hilo, Cosmas Mseti, Kaimu Mkuu wa Mauzo Vodacom Kanda ya Ziwa, Ahmed Akbarali, Meneja wa Vodacom Kanda ya Ziwa, Victoria Chale. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wagombea udiwani 24 warejeshwa

**Na Mwandishi Wetu**

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imepitia, kuchambua na kufanyia kazi rufani 46 za wagombea udiwani ambao hawakuridhika na uamuzi wa wasimamizi wa uchaguzi kutokana na pingamizi zilizowasilishwa dhidi yao na kukubali kuwarejesha 24.

Kwa mujibu wa taarifa kwa vyombo vya habari iliyotolewa jana na Mkurugenzi wa Uchaguzi wa NEC, Dk. Wilson Mahera, rufani 22 zimekataliwa.

Alizitaja kata zilizokubaliwa rufani na majimbo kwenye mabano kuwa ni Dunda (Bagamoyo), Mtwivila (Iringa Mjini), Kikilo (Kondoa), Makurumla (Ubungo), Hezya (Vwawa), Makorongoni (Iringa Mjini) na Bwawani (Arumeru Magharibi).

Nyingine ni Jinjimili (Magu), Kimnyaki (Arumeru Magharibi), Lemanyata (Arumeru Magharibi), Mkwawa (Iringa Mjini), Kisarawe II (Kigamboni), Makurumla (Ubungo), Mbabala (Dodoma Mjini), Mpanda Hoteli (Mpanda Mjini).

Lusungo (Kyela), Same (Same), Maisaka (Babati Mjini), Makuburi (Ubungo), Kibada (Kigamboni), Maore (Same Mjini) na rufani tatu kutoka kaya ya Mshindo (Iringa Mjini).

Pia NEC imekataa rufani 13 za wagombea udiwani ambao hawakuteuliwa, kata na majimbo kwenye mabano kuwa ni Kawanjense (Mpanda), Mjini Chorombola (Ulanga), Mabokweni (Tanga Mjini), Chanika (Karagwe), Mwamala (Manonga) na Kiomboi (Iramba Magharibi). Nyingine ni Mwasenkwa (Mbeya Mjini), Old Iranga (Iramba Magharibi), Magara (Babati Vijijini), Arri (Babati Vijijini), Chapwa (Tunfuru) na mbili kutoka Kaya ya Kibamba (Kibamba).

Vile vile, taarifa hiyo ilisema kuwa rufani tisa za kupinga walioteuliwa ni Nonde (Mbeya Mjini), Mwagata (Iringa Mjini), Mabibo (Ubungo), Mkimbizi (Iringa Mjini), Kipanga (Sikonge), Nsoho (Mbeya Mjini), Ilmela (Mbeya Mjini), Bagara (Babati Vijijini) na Nkinga (Manonga).

Pia Tume hiyo imefanyia kazi rufani 113 za wagombea ubunge. Rufani 149 za udiwani zimefanyiwa kazi ikiwamo zilizotolewa maamuzi mwishoni mwa wiki kwa madiwani 24.

# Waziri Mkuu: Tutaanzisha mamlaka za maji Chemba

**Na Mwandishi Wetu**

MJUMBE wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema serikali inapanga kuanzisha Mamlaka ya Maji Chemba hivi karibuni.

Alitoa kauli hiyo jana wakati akizungumza na wananchi katika eneo la Mnadani, Kijiji cha Kelema, Kata ya Paranga, Wilaya ya Chemba mkoani Dodoma kwenye mkutano wa kumwombea kura Rais John Magufuli na mgombea ubunge Jimbo la Chemba, Mohammed Moni na wagombea udiwani wa CCM.

"Wilaya hii haina mamlaka ya maji. Kwa hiyo tutaanzisha Mamlaka ya Maji ili watumishi wawepo wilayani. Wasimamie kwa karibu na waweze kufuatilia vyanzo vya maji kutokea hapa Chemba wakati tukiendelea kutatua tatizo la maji wilayani hapa. Tutaunda Mamlaka ya maji hivi karibuni."

Alisema serikali ilitoa Sh. bilioni 1.688 za kutafuta vyanzo vya maji huko Orada, Kisanga, Moi, Mondo na Ndaki. "Pia Serikali ya Awamu ya Tano imetoa Sh. milioni 677 za kuchimba visima huko Mondo, Mrijo Juu, Chambalo, Hamai na Chemba."

"Tuna uhakika tukipata lita za maji za ujazo 4,700 zinatosha kabisa kujenga mtandao wa maji. Kazi ya kuboresha miundombinu ya maji inaendelea. Zimetengwa fedha nyingine, Sh. milioni 150 za kusambaza maji Kelema, Msaada na Bumbu."

Akizungumzia sekta ya afya, Majaliwa alisema zimetolewa Sh. bilioni 1.8 za kujenga Hospitali ya Wilaya ya Chemba ili wananchi wapate huduma za tiba wakiwa hapohapo badala ya kwenda Kondoa kama ilivyokuwa awali.

"Nia yetu ni kuhakikisha kila Mtanzania anapata huduma hukohuko aliko kwa kuweka zahanati katika kila kijiji, vituo vya afya kwa kila kata. Wakimaliza ujenzi, tumetenga Sh. milioni 500 za vifaa vya hospitali kwa majengo yote saba."

"Tumepeleka Sh. milioni 400 za kituo cha afya kule Hamai, Sh. milioni 500 Mrijo na Sh. milioni 400 Kwa Mtoro. Kazi ya ujenzi ikiisha, kila kimoja kitapata Sh. milioni 250 za vifaa tiba."

Ninawaomba mumpe kura Rais Dk. Magufuli, mbunge na madiwani wa CCM ili tukamilishe kazi hizi kwa sababu serikali hii ni ya watekelezaji. Tunasema na tunatenda."

Wakati huohuo, Majaliwa amesema Rais Magufuli anataka umeme usambazwe kote nchini na ndiyo maana akaamua kupunguza bei ya kuunganisha umeme.

"Rais wetu kasema anataka kuona kila nyumba ya Mtanzania inawaka umeme. Amepunguza gharama za kuunganisha umeme kutoka Sh. 380,000 hadi Sh. 27,000. Rais wetu kasema ni marufuku kulipia nguzo za umeme. Mwananchi hutakiwi kulipia nguzo yoyote ile. Atakayekuuzia nguzo, mwambie akupe risiti, leta risiti tumlipue huyo ofisa," alisisitiza.

Majaliwa anaendelea na mikutano ya kuomba kura wilayani Kondoa.

HABARI KITAIFA

# Afungwa miaka 30 jela kubaka mtoto

**Na Jumbe Ismailly,** SINGIDA

MKAZI wa Kijiji cha Bukatika Kata ya Matongo katika Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, Shabani Salimu (25), amehukumiwa na Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Singida kutumikia adhabu ya kifungo cha miaka 30 jela baada ya kutiwa hatiani kwa kosa la kumbaka binti mwenye umri wa miaka 13.

Katika shauri la jinai namba 135/2019 ilidaiwa na Mwanasheria wa Serikali, Elizabeth Barabara, kwamba mshtakiwa alitenda kosa hilo Juni 16, 2019 saa 9:00 mchana katika Kijiji cha Bukatika, Kata ya Matongo wilayani Ikungi. Aidha, mwanasheria huyo alidai pia kwamba siku ya tukio binti huyo alikuwa ameenda kutafuta kuni na ndipo wakati akirejea nyumbani alikutana njiani na mshtakiwa, ambaye alimvuta na kumwingiza vichakani kisha kumbaka.

Kwa mujibu wa Barabara, wakati binti huyo alipokuwa akivutwa kupelekwa vichakani alijaribu kupiga kelele za kuomba msaada kwa wasamaria wema, lakini haikuwezekana kupata msaada, hali iliyomsaidia mshtakiwa huyo kumaliza matamanio yake.

Hata hivyo mwanasheria huyo alidai kuwa katika maelezo aliyotoa mshtakiwa kituo cha polisi alikiri kwamba alimtendea unyama binti huyo na alipofikishwa mahakamani alikana.

Hata hivyo, baada ya Salimu kukataa kutenda kosa hilo ndipo upande wa mashtaka ulipeleka mahakamani mashahidi kumi, walitoa ushahidi ambao haukutia shaka yoyote kuwa mshtakiwa ndiye aliyembaka binti huyo na ndipo mahakama ilipomtia hatiani.

Kabla ya kutoa hukumu kwa mshtakiwa huyo, Hakimu Mkazi Mwandamizi wa Mahakama ya Mkoa wa Singida, Robert Oguda, alisema vitendo vya ubakaji katika jamii vimezidi kushika kasi.

Hakimu Oguda alisisitiza kuwa ili liwe fundisho kwa watu wengine wenye tabia kama ya mshtakiwa huyo, mahakama hiyo ina muhukumu mshtakiwa adhabu ya kutumikia kifungo cha miaka 30 jela.



Mratibu wa Mradi wa Usimamizi shirikishi wa rasilimali za uvuvi Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (SWIOfish), wilayani Mkinga, mkoani Tanga, Asha Churu (wapili kulia), akieleza jambo kwa viongozi wa Serikali ya Kijiji cha Zingibari na kikundi cha ulinzi shirikishi wa rasilimali za uvuvi (BMU) baada ya kufanya ukaguzi wa ujenzi unaoendelea wa ofisi ya BMU kijijini hapo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# DC Gondwe aandaa jukwaa kutatua kero

**Na Elizabeth Zaya**

MKUU wa Wilaya ya Temeke, Godwin Gondwe, kwa kushirikiana na manispaa hiyo, wameandaa jukwaa la kutatua kero za wananchi kwa siku 14 linalotarajiwa kuanza leo.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, Gondwe alisema jukwaa hilo litashirikisha taasisi zote za serikali ambazo zitaweka kambi katika viwanja vya Zakhem na Mwembe Yanga kwa ajili ya kusikiliza na kutatua kero zitakazopelekwa na wananchi.

"Jukwaa hili linajulikana kama 'One Stop Jawabu-Temeke 2020', na ni utekelezaji wa agizo la Rais John Magufuli ambaye amesema wateule wake na watumishi wote wa umma watatue kero za wananchi," alisema Gondwe.

Gondwe alisema taasisi 30 zinatarajia kuwapo katika viwanja hivyo kwa ajili ya kusikiliza na kuwahudumia wananchi.

"Tunataka hizi taasisi ambazo zitakuwapo katika viwanja hivi zisikilize, kuhudumia, kutatua na kutoa majawabu ya changamoto za wananchi papo kwa papo," alisema Gondwe.

Alitaja baadhi ya taasisi zitakazokuwapo ni NIDA, RITA, BRELA, TRA, NSSF, NHIF, NHC, na DAWASA.

Nyingine alisema ni Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete, Hospitali ya Rufani Temeke, Uhamiaji, taasisi za kifedha pamoja na idara zote za halmashauri ya manispaa hiyo.

Mkurugenzi wa Manispaa hiyo, Lusubilo Mwakabi, alisema wanaamini kwamba jukwaa hilo litasaidia kwa kiwango kikubwa kutatua kwa wingi changamoto ambazo zimekuwa zikisumbua wananchi.

# Vichwa vikubwa, mgongo wazi tatizo kwa watoto

**Na Christina Mwakangale**

TAASISI ya Mifupa Muhimbili (MOI), inapokea watoto 700 hadi 1,200 kwa mwaka walio na tatizo la vichwa vikubwa na mgongo wazi, ambao chanzo cha matatizo hayo ni lishe duni kwa mama zao wakati wa ujauzito.

Daktari Bingwa wa Upasuaji wa Ubongo, Mgongo na Mishipa ya Fahamu MOI, Dk. Laurent Mchome, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam katika mahojiano na redio moja kuhusu watoto wenye tatizo hilo nchini.

Dk. Mchome alisema tatizo hilo lipo kwa kiwango kikubwa na kwamba mwaka jana watoto walifika MOI kwa matibabu wenye vichwa vikubwa walikuwa ni 886 kati yake 174 wenye vichwa maji na mgongo wazi ni 69.

"Kati ya watoto 100 wanaozaliwa watoto wawili hadi watatu wana uwezekano wa kuzaliwa na tatizo la mgongo wazi au kichwa maji. Na tatizo lao sababu linatokana pengine kabla ya kuzaliwa yaani wakiwa tumboni au baada ya kuzaliwa," alifafanua Dk. Mchome.

Bingwa huyo alisema kuwa watoto wanaowapokea MOI, tatizo lao hutokea tangu wakiwa tumboni mwa mama zao au baada ya kuzaliwa, iwapo mtoto atapata jeraha kichwani litakalosababisha damu kuganda katika ubongo.

"Tatizo huanzia tumboni mwa mama zao kabla ya kuzaliwa katika kipindi cha miezi mitatu ya ujauzito, iwapo mama mjamzito atatakosa madini ya chuma na lishe bora," alisema Dk. Mchome.

Alisema kundi lingine la watoto wenye matatizo hayo ni wale ambao baada ya kuzaliwa walipata majeraha kwenye ubongo na damu kuivilia ndani kutokana na ajali au kuanguka.

"Awali ilikuwa tunapokea watoto wenye tatizo hili kutoka Morogoro maeneo ya Ifakara, Mahenge au Kanda ya Kati haikufahamika ni kwanini, lakini hivi sasa wagonjwa hao wanatoka mikoa mbalimbali nchini," alieleza bingwa huyo.

Alisema dalili ya watoto wenye tatizo la mgongo wazi ni kuwa na nundu mgongoni na kupata shida ya haja ndogo na hata kushindwa kutembea na kwamba wakipata tiba mapema, hupona.

Dk. Mchome alitoa wito kwa wanawake na kinamama walio na matarajio ya kupata ujauzito kuwa na lishe bora, kufika kliniki mwezi wa kwanza wa ujauzito pamoja na kutumia dawa zenye madini ya chuma kwa ushauri wa daktari.

Siku ya watoto wanaozaliwa na vichwa vikubwa na mgongo wazi duniani, huadhimishwa Oktoba 25 kila mwaka, ili kuongeza uelewa kwa jamii kuhusu tatizo hilo.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Makocha waachwe huru kuamua, kupanga kikosi

**BAADA** ya mechi nyingine kuchezwa kuanzia Ijumaa, Jumamosi na jana Jumapili, raundi ya pili ya Ligi Kuu Bara itakamilika leo kwa kuchezwa mechi moja pale Uwanja wa Majaliwa mkoani Lindi, kwa wenyeji Namungo FC kuwakaribisha Polisi Tanzania ya Kilimanjaro.

Ligi hiyo ambayo msimu huu mpya wa 2020/21, inashirikisha timu 18 tofauti na uliomalizika ambao ulikuwa na timu 20, imeanza kwa timu kuonyesha zimepania kuvuna pointi za mapema katika mzunguko huu wa kwanza.

Hata hivyo, presha kutoka kwa mashabiki na baadhi ya viongozi tayari zimeanza kuwa kubwa zikielekezwa kwa makocha, wakiwataka kuwapanga baadhi ya wachezaji wanaowataka katika vikosi vyao.

Presha hiyo inatokana na baadhi ya klabu kufanya usajili mkubwa, hivyo wanachotaka ni kuwaona nyota hao wakipangwa katika kikosi cha kwanza na kuanza kuwashuhudia, lakini imani yao kubwa wakiamini wanaweza kuchangia ushindi wa mabao mengi.

Nipashe tunatambua zipo baadhi ya klabu ambazo zimefanya usajili wa nyota wengi wapya, lakini zikafanya mabadiliko makubwa katika mabenchi yao ya ufundi kwa kuteua makocha wapya, ambao ndio kwanza wanaanza kuunda vikosi vya ushindani kwa kuingiza mifumo na mbinu zao.

Lakini hata kwa baadhi ya klabu ambazo hazikubadili mabenchi yao ya ufundi, bado makocha wanahitaji muda kuweza kutengeneza uelewano ('chemistry') ya kikosi kwa nyota wapya kuzoeana kwanza na wenzao kabla ya kuanza kupata nafasi mara kwa mara katika kikosi cha kwanza.

Kabla ya Yanga kuivaa Mbeya City katika Uwanja wa Mkapa jana, kwenye mechi yao ya awali wakati ikitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Tanzania Prisons, mashabiki wengi wa timu hiyo ya mtaa wa Twiga na Jangwani, ni miongoni mwa ambao hawakufurahishwa na kikosi kilichopangwa na Kocha wao Mkuu, Mserbia Zlatko Krmpotic.

Licha ya kufurahishwa na kasi ya mchezo huo, bado lawama na malalamiko yalikuwa mengi kutoka jukwaani na baada ya mechi, wakitamani baadhi ya wachezaji wageni wangeanza akiwamo kiungo Muangola Carlos Carlinhos.

Katika hilo, si kwa Yanga pekee, bali hata kwa watani zao Simba, mashabiki wamekuwa wakitoa presha kubwa kwa Kocha Mkuu, Sven Vandenbroeck wakimtaka kubadili mfumo wa kuanza na mshambuliaji mmoja kwa kutumia mfumo utakaowezesha timu hiyo kuwa na washambuliaji wawili mbele.

Presha kwa Sven kwa sasa inaonekana kutokuwa kubwa sana kwa sababu tu, timu hiyo haijapoteza mchezo wowote msimu huu, lakini sare ya juzi dhidi ya Mtibwa Sugar ilianza kuibua maneno, jambo ambalo tunaamini siku ikipoteza vuguvugu hilo litakuwa kubwa kwake, pengine tofauti na hali ilivyo sasa.

Lakini kikubwa mashabiki, wadau na kwa baadhi ya viongozi wa soka, hawana budi kutambua mpira wa miguu siku zote una matokeo matatu, kushinda, kushindwa na sare, pia kila timu inaposhuka uwanjani huwa na mbinu zake lengo likiwa moja tu, kupata matokeo.

Hivyo, kama ilivyo wakati timu inaposhinda hufurahi pamoja, basi inapopoteza pia mashabiki hawana budi kuyapokea matokeo hayo pamoja, huku wakifahamu pia wamezidiwa mbinu na kuadhibiwa kutokana na makosa timu iliyofanya.

Nipashe tunaamini makocha ndio wanaoishi kikosini na wachezaji wakati wote, hivyo wanawafahamu vema nje ndani na hata kisaikolojia, jambo ambalo wanapaswa kuachwa huru kupanga na kuamua nani aanze na acheze kwa wakati gani kutokana na hali ya kila mchezaji kutegemeana na mchezo wenyewe.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Kumbughudhi Mo kwa sasa ni kulisaliti soka letu

**BAADA** ya kutangazwa kwa mwanamama Barbara Gonzalez kuwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa Klabu ya Simba, kukazuka maneno mengi ambayo mengine yalienda mbali sana na kuonekana kuna kitu ndani yake na wala si mambo ya kimichezo.

Gonzalez alichaguliwa na Bodi ya Klabu ya Simba kushika wadhifa huo baada ya Senzo Mbatha kutimkia Klabu ya Yanga.

Haijulikani ni kwa sababu ni mwanamke, au vipi, kwani kuna watu walikuja juu na kuanza kuhoji sifa zake za kuongoza, kiwango chake cha elimu, lakini uzoefu wake kwenye soka. Wakati watu waliokuwa wakihoji hivyo, walipokuwa wakijibiwa hoja baada ya hoja na kugundua kuwa Gonzalez ana sifa ya vitu vyote hivyo ambavyo viliulizwa, tena kwa kiwango cha hali ya juu, huku akipongezwa na kada mbalimbali za ndani na nje ya nchi, ikiwamo Ubalozi wa Marekani, Shirikisho la Soka Afrika (Caf) na hata Rais mwenyewe wa Shirikisho hilo, Ahmad Ahmad naye akimpongeza mwanamama huyo yeye binafsi.

Na wakati baadhi ya taasisi nyingi duniani zikipongeza uteuzi wa Simba kwa mwanamama huyo, kuna watu wachache walionekana kupinga.

Lakini baada ya kuona hali inageuka, wapingaji hao wakahamia kwa Mwekezaji wa Simba, Mohamed "Mo" Dewji kuulizia ni kwa nini hajaingiza pesa kiasi cha Sh. bilioni 20 kwenye akaunti ya Simba?

Hapa unaanza kujiuliza, hoja ni Gonzalez, au ni Sh. bilioni 20? Unashindwa kupata jibu.

Hakuna mtu yeyote asiyefahamu kuwa pesa hizo hazijaingizwa na sababu zimekuwa zikitolewa wazi mara kwa mara, sasa kwa nini swali hilo linaulizwa tena kipindi hiki baada ya mwanamama huyo kuwa Ofisa Mtendaji Mkuu?

Baadhi wanasema Barbara ametoka kwenye makampuni au taasisi za Mo, hivyo hataweza kuhoji Sh. bilioni 20, hapo unajiuliza kama kwenye kazi ya Ofisa Mtendaji Mkuu ni kuhoji pesa, au kufanya kazi za klabu?

Ninavyojua kazi ya kuhoji pesa ni ya wanachama, tena kwenye mikutano rasmi ya klabu na wala si ya Ofisa Mtendaji Mkuu. Na ndiyo maana hata Senzo alipokuwa kazini hakuwahi kuhoji hizo pesa, iweje eti Barbara ndiye atatakiwa kuhoji?

Halafu unajiuliza, hivi hizo pesa ambazo baadhi ya watu wanalalamika kuwa hajaweka, aziweke kwenye akaunti gani? Maana taarifa zinaeleza taasisi za kiserikali na kifedha, bado hazijamaliza uhakiki wa madeni na mambo mengine, kabla ya kuruhusu kufunguliwa akaunti ambayo itatakiwa kiasi hicho kiwekwe.

Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya Simba, Crescentius Magori hivi majuzi aliwahakikishia wanachama na mashabiki wa Simba kuwa taasisi hizo zikishamaliza uhakiki kila kitu kitakwenda sawa kwa sababu pesa hizo zipo na wanachosubiri ni kukamilika tu kwa mchakato huo. Kwa hapa mimi sioni tatizo, kwa sababu si Mo anayechelewesha hili. Ningewaelewa Simba endapo wanalalamikia hili kama mwekezaji angekuwa amekaa pembeni anasubiri mchakato wote ukamilike, ndiyo aanze kazi.

Lakini Mo kabla hata ya mchakato wote kukamilika kwa asilimia 100, amekuwa akiihudumia klabu na timu kwa ujumla, kiasi kwamba Simba imekuwa moja ya timu kivutio kwa sasa si Afrika Mashariki na Kati tu, bali Afrika nzima.

Hivyo, ninachoamini ni kwamba kwa sasa kumbughudhi Mo kwa ni sawa na kutaka kulisaliti ama kulitia doa soka la Tanzania kwa sababu linahitaji watu wengine zaidi ya yeye na uwapo wake Simba unazidi kuzifanya klabu zetu nyingine kuwa imara, na hilo tumeanza kulishuhudia msimu huu.

Ikumbukwe hadi sasa, ni yeye pekee ndiye aliyekubali kuwekeza kwenye klabu ya mpira wa miguu, huku matajiri wengine wakionekana kukataa na kusitasita kufanya hivyo huku wakidai si waumini wa mfumo wa uendeshaji wa klabu kwa njia ya hisa. Nadhani kwanza wanamwangalia Mo atafika wapi. Inawezekana baada ya kuona Simba imesonga mbele na kufanikiwa, watajitokeza matajiri wengine kuwekeza kwenye klabu zingine kama Yanga, Ndanda FC, KMC na zingine nyingi, lakini walio na maneno maneno na mambo ya kutaka kumkatisha tamaa Mo, ninafahamu hawatojitosa na soka letu litaendelea kudidimia.

Wala tusidanganyane, soka la sasa duniani linahitaji pesa na wala si ya wanachama kuchangishana, au ujanja ujanja kama ambavyo tuliona ile kampeni iliyoitwa "Kubwa Kuliko", iwapi sasa? Wakati hata baadhi ya matajiri walioahidi bado hawajakamilisha ahadi zao!

Mo mwenyewe binafsi anaonekana kupenda sana soka, klabu yake ya Simba na Taifa Stars, ndiyo maana pamoja na changamoto na kupigwa madongo na baadhi ya watu bado ameendelea kukomaa tu huku akiahidi "kamwe hataiacha Simba", lakini ingekuwa kwa matajiri wengine ambao 'hawana ngozi ngumu', tungewakimbiza kwenye soka na kuendelea kubaki kama lilivyo.

Kama alivyosema Magori kuwa wapo watu ambao hawana nia nzuri na klabu, kwani hata mchakato ukikamilika na pesa ikaingizwa, wanaweza kuibuka na lingine jipya.

Mimi nadhani wadau wa soka wanatakiwa wampe ushirikiano Mo, ili kuwavutia matajiri wengine wajiingine kwenye soka, vinginevyo anaweza kubaki Mo tu peke yake miaka nenda rudi, kitu ambacho hakitokuwa na afya kwenye soka la Tanzania.

# CUF kuwekeza kwenye afya, elimu

**Na Boniface Gideon,** IRINGA

CHAMA cha Wananchi (CUF), kimesema endapo kitapata ridhaa ya kuongoza nchi kitawekeza kwenye rasilimali watu ikiwamo afya na elimu.

Mgombea urais kupitia chama hicho, Profesa Ibrahim Lipumba, alitoa ahadi hiyo wakati akihutubia wananchi wa Wilaya ya Kilolo, mkoani Iringa.

Alisema kama watu hawana elimu na afya bora ukiwekezaji kwenye vitu hautawasaidia chochote.

Profesa Lipumba aliikosoa Serikali ya CCM kwa uwekezaji wa kununua ndege badala ya miundombinu muhimu ya afya na elimu.

"Endapo tutapewa ridhaa Sera ya CUF itawekeza kwenye vitu muhimu vya afya na elimu ili viweze kuja kuwasaidia Watanzania kujikwamua na umaskini," alisema na kuongeza:

"Kama taifa lazima tuwe na utaratibu wa kuhakikisha watoto wanapata lishe bora ili kujijengea kinga ya mwili na serikali ina kila sababu ya kuhakikisha wanapata elimu bora."

Prof. Lipumba alisema muungano ni muhimu na endapo watachaguliwa watauimarisha kati ya Tanzania Bara na Zanzibar na kuwa na haki sawa kwa pande zote mbili.

Alisema wanahitaji kuleta mabadiliko ili panapokuwa na mzunguko wa fedha na kwamba wananchi wa Kilolo ni watu wanaojishughulisha na kilimo, lakini hawana msaada wowote wanaoupata kutoka serikalini.

"Tunaomba kura zenu, zamani Iringa ilikuwa 'Big four' katika uzalishaji wa mahindi wananchi ni wachapa kazi, lakini hawajajengewa mazingira ya kuutokomeza umaskini," alisisitiza.

"Tunaomba kura zenu ili biashara zitoke na uwekezaji uongezeke vitunguu vipate soko sio tu Tanzania mpaka Afrika Mashariki, yote watu wapewe utaalamu wa kuongeza tija katika shughuli zao za kilimo...wapate zana za kumwagilia na za kilimo."

Alisema unapoongeza tija kwenye kilimo ndipo unapopata uwezo wa kuendeleza viwanda kwa kuwa kilimo kinatoa chakula.

Kwa upande wake mgombea mwenza Hamida Abdalah Huweishi, aliwataka vijana wasijutie kuzaliwa kwa kuwa muda uliopita siyo muafaka kwa kuwa CUF itawaboresha katika kila aina ya sekta kwa kutumia rasilimali za nchi zilizopo.




Balozi wa Kiss Kondomu nchini, Idris Sultan (kushoto), akizungumza na wageni waalikwa wakati wa uzinduzi wa kondomu mpya ya kiume Kiss jana, jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wadau sekta binafsi waomba kupitiwa upya sheria ya TASAC

**Na Mwandishi Wetu**

WADAU wa Sekta Binafsi nchini (TPSF), wameiomba serikali kupitia upya sheria iliyoanzisha Shirika la Wakala wa Meli Tanzania (TASAC) ili kuondoa changamoto zinazowakabili wafanyabiashara hapa nchini.

Akizungumza jijini Dar es Salaam baada ya mkutano uliowakutanisha wadau wa sekta binafsi na wawakilishi kutoka serikalini, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa TPSF, Zachy Mbenna, alisema TPSF imewaleta pamoja wadau wa sekta hiyo na umma ili kutoa mapendekezo ya nini kifanyike kuboresha huduma za utoaji mizigo na forodha katika Bandari ya Dar es Salaam.

"Tumekuwa na majadiliano muhimu kati ya wafanyabiashara wanaotoa huduma za mizigo na forodha katika Bandari ya Dar es Salaam, tunashukuru kwa kuwa tumeweza kutengeneza nafasi kwa wadau wetu kukutana na wenzetu wa serikali jambo ambalo litasaidia kuondoa baadhi ya changamoto," alisema Mbenna.

Alisema kumekuwa na mazingira mazuri ya kimawasiliano kati ya TPSF na serikali katika kushughulikia changamoto za ufanyaji biashara hapa nchini hali inayowaweka wafanyabiashara kwenye wakati mzuri wa kutoa huduma kwa Watanzania.

"Siku za nyuma hali ilikuwa tofauti na ilivyo sasa, kumekuwa na ushirikiano mkubwa kati ya taasisi ya sekta binafsi na ile ya umma katika masuala yote muhimu yanayohusu biashara na uwekezaji. Tunaamini mkutano huu utazidi kuleta matokeo mazuri kwa kuwa sekta binafsi ni uti wa mgongo katika kusogeza maendeleo ya Taifa husika," alisema.

Kwa upande wake Katibu Mtendaji wa TASAC, Abel Uronu, alisema mabadiliko katika uendeshaji wa TASAC ni muhimu kufanyika ili kukidhi haja ya Watanzania kwa kuzingatia gharama, wepesi na utaalamu wa kufanya biashara ndani ya nchi.

"TASAC inadhibiti na pia inafanya kazi ya uwakala kwa wakati mmoja, tunaiomba serikali iweze kuangalia sheria iliyoanzishi TASAC mwaka 2017 ili kurahisisha utoaji wa huduma na kuondoa hatari ya kuwa na mgongano wa kimaslahi," alisema Uronu.

Naye Rais wa Chama cha Usafirishaji wa Mizigo nchini (TAFFA), Edward Urio, amesema kuwa iwapo serikali itashindwa kufanya mapitio upya ya sheria iliyoanzisha TASAC, itapelekea kukosa kodi kwa kuwa kampuni zaidi ya 800 zitashindwa kujiendesha na hatimaye kufungwa.

"Tunaamini serikali itasikiliza maoni yetu na kufanyiwa marekebisho ya sheria hiyo ili kuendelea kuzalisha ajira kupitia kampuni zaidi ya 800 zinazojihusisha na uwakala wa meli na forodha na pia upatikanaji wa kodi ambayo itasaidia uendeshaji wa serikali," alisema.

Yosepha Tamam, mwakilishi wa timu kutoka Wizara ya Fedha, alisema changamoto na mapendekezo yaliyotolewa katika mkutano huo zitafikishwa serikalini kuangalia namna nzuri ya kuwafanya ili mazingira ya ufanyaji wa biashara hiyo yawe rafiki kwa kila mdau.

# SUA kuwawezesha waganga tiba asili

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WATAFITI wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA ) kutoka Idara ya Kemia na Fizikia, wamepongezwa kwa jitihada za kuwajengea uwezo waganga wa tiba asili na tiba mbadala kwa kuongeza thamani ya dawa zao na matumizi endelevu ya miti dawa ili kuboresha tiba na kuongeza kipato.

Kaimu Mganga Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Dk. David Ntahindwa, alitoa pongezi hizo mjini Njombe wakati akifungua mafunzo kwa waganga hao wa tiba asili na Tiba mbadala wa Mkoa wa Njombe.

Mafunzo hayo yaliendeshwa na SUA kupitia mradi wa uvumbuzi katika mimea dawa kwa ustawi wa Watanzania (GRILI), kwa kushirikiana na mradi wa kuongeza thamani kwa kemikali za SG kwa matibabu ya magonjwa ya binadamu na wanyama (vaSPHAD).

Dk. Ntahindwa, alisema katika kipindi cha hivi karibuni dawa asili na tiba mbadala zimepata umaarufu mkubwa kutokana na watu wengi kuanza kuzitumia kwa ajili ya kutibu magonjwa mbalimbali.

Alisema, pamoja na matumizi hayo, lakini mazingira ya utengenezaji na matumizi bado hayajawekwa sawa, na hivyo kuwafanya watu wengine kusita kuzitumia kwa kuhofia usalama wao.

Dk. Ntahindwa, alisema mafunzo hayo yamekuja muda muafaka hasa wakati ambao serikali inasisitiza na kuzipa kipaumbele dawa za asili ili kutibu magonjwa mbalimbali ambayo yanaweza kutibika na dawa za nchini badala ya kutegemea dawa kutoka nje ya nchi wakati zinatoka kwenye miti na mimea ambayo ipo nchini.

Naye Mkuu wa mradi wa GRILI, Dk. Faith Mabiki, alisema umefika wakati waganga wa tiba asili na tiba mbadala kunufaika na kazi zao wanazozifanya kwa kutibu jamii.

Alisema hilo litawezekana endapo waganga hao wataongeza thamani ya dawa zao na kushiriki kwenye kulima miti dawa hiyo, ili isipotee kwa kuwa kwa sasa wanaivuna kila siku.

Alisema kuna dawa nyingi zinatoka nje ya nchi hasa China na kutibu watu huku zikiwa zimeboreshwa vizuri wakati miti iliyotumika pia ipo nchini.

Dk. Mabiki, alisema kwa kuwa mahitaji ya miti dawa yanaongezeka siku hadi siku kuna uwezekano wa miti mingi kupotea, hivyo mradi na watafiti wanaona kuna umuhimu wa waganga hao kuanza kulima kilimo cha miti dawa na mimea dawa ambayo ni muhimu katika kutoa tiba na hivyo kusaidia kurahisha upatikanaji wake.

Kwa mujibu wa mkuu wa mradi huo, waganga wa tiba asili na tiba mbadala zaidi ya 20 na viongozi wao wa wilaya zote za Mkoa wa Njombe walifundishwa kanuni za msingi za usindikaji wa dawa, athari za usugu wa dawa, kemikali zinazopatikana kwenye mimea dawa mbalimbali nchini na pia namna ya kupanda mimea dawa hiyo katika mashamba na kustawisha.

# Kimei ataka Himo kuwa makao makuu ya Halmashauri ya Moshi

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

MGOMBEA ubunge wa tiketi ya CCM), Jimbo la Vunjo, Moshi Vijijini, Dk. Charles Kimei, amewaomba wananchi wa jimbo hilo kumpa ridhaa ya kuwa mbunge wao ili aweze kuwaletea mapinduzi ya kiuchumi.

Aliyasema hayo katika mkutano wa uzinduzi wa kampeni zake uliofanyika katika Mji Mdogo wa Himo na kuratibiwa na Waziri Mkuu mstaafu Mizengo Pinda, na kuhudhuriwa na maelfu ya wakazi wa jimbo hilo.

Dk. Kimei alisema kuwa jimbo hilo lina changamoto nyingi ikiwamo miundombinu mibovu ya barabara, elimu, afya na ukosefu wa masoko thabiti kwa mazao yazalishwayo na wakazi wa jimbo hilo.

Alisema ikiwa wananchi watamchagua kuongoza jimbo hilo, atatumia uzoefu wake katika sekta ya fedha, kuanzisha Mfuko wa Ujasiriamari wa Jimbo ambao utahusika kutoa mikopo nafuu kwa wananchi ili kuwapa mitaji na hivyo kuwajengea uwezo wa kujiajiri na kuajiri na kuwapaisha kiuchumi.

"Kwa kushirikiana na wadau wengine, tunakamilisha mchakato wa kuanzisha mfuko wa wajasiriamari Vunjo. Mimi mwenyewe nitatoa andiko la mradi ili kupata fedha za uwezeshaji wa makundi maalum ya wakulima, wafugaji, vijana, wanawake, bodaboda na mafundi makenika kwa kuwapa mikopo nafuu," alisema.

Kuhusu kilimo na mazao ya shamba, alizungumzia kuhusu kuanzishwa kilimo cha umwagiliaji ili kuongeza tija, sambamba na kuwawezesha wananchi kuanzisha viwanda vya usindikaji hivyo kuongeza thamani ya mazao.

"Jambo kubwa la msingi ni kuanzisha viwanda vya usindikaji ili kuongeza thamani ya mazao yetu. Badala ya kuuza mpunga, tutaanza kuuza mchele wetu uliofungwa vizuri. Badala ya kuuza nyanya ambazo huharibika kirahisi, viwanda hivi vitasindika nyanya hizo na tutauza tomato paste yetu wenyewe, hivyo kuongeza thamani na vipato vya wananchi wa Himo. Tutafanya hivyo pia kwa mazao ya Kahawa na mengineyo," alisema Dk. Kimei.

Aliongeza kuwa, eneo lingine ni kuboresha miundombinu ya barabara ili kurahisisha usafarishaji wa mazao hayo, ili kufikia masoko kwa urahisi kutokana na hali hiyo, maisha ya wananchi yatabadilika na kupiga hatua za kimaendeleo.

Kwa upande wa changamoto sekta ya afya, alisema kuwa vituo vingi vya afya vinahitaji ukarabati mkubwa wa haraka, huku vikikosa vifaa vya kisasa kama XRAY na Ultra Sound.

"Tutasimamia kukamilisha ujenzi wa hospitali ya Wilaya ya Himo ambao ulisimama. Pia tutashughulikia masuala ya bima za afya na matibabu kwa wazee."

Kuhusu ukosefu wa gari la wagonjwa, Dk. Kimei alisema 'Kwa sasa, jimbo letu halina gari la uhakika la kubebea wagonjwa, Naahidi kutoa gari langu mimi mwenyewe, lifanye kazi hiyo wakati tunaendelea na mchakato wa kuongeza mengine," alisema.

"Nimejipanga kuhakikisha wananchi wa Himo wanapata maendeleo kama inavyosema ilani ya Chama Cha Mapinduizi. Nitashirikiana na serikali kila nyanja ili kuhakikisha wananchi wanapata maendeleo na kunufaika na rasilimali zao." Alisema.

Pia Kimei alimwombea kura mgombea wa urais wa CCM, Rais John Magufuli pamoja na madiwani wa CCM ndani ya Jimbo la Vunjo.




Waziri Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, akimnadi mgombea ubunge kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Jimbo la Vunjo, Moshi Vijini mkoani Kilimanjaro, Dk .Charles Kimei, katika mkutano wa uzinduzi wa kampeni zake uliofanyika katika Mji Mdogo wa Himo mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mgombea CHADEMA ajinadi kufuata njia za Mwakyembe

**Na Thobias Mwanakatwe,** KYELA

MGOMBEA ubunge Jimbo la Kyela kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Alinanuswe Mwalwage, ameanza kunadi sera zake kwa kutumia miradi mikubwa iliyotekelezwa na Mbunge wa Jimbo hilo anayemaliza muda wake, Dk. Harrison Mwakyembe.

Akizungumza kwa nyakati tofauti katika mikutano mbalimbali ya kampeni aliyoifanya katika kata saba za jimbo hilo, alisema Dk. Mwakyembe kama binadamu anaweza kuwa na upungufu, lakini katika suala la kuleta maendeleo Kyela ameifanya kazi vyema.

"Tangu utawala wa serikali ya awamu ya nne, Dk. Mwakyembe, amekuwa akiteuliwa kuwa waziri, sasa wewe mwananchi unawezaje kusema ni mbovu, ili iweje, najua wale wanaomsema ovyo kule ni minyukano tu ya kura za maoni ndio inayoendelea, lakini ukweli utabaki pale pale amefanya maendeleo makubwa," alisema.

Mwalwage alitaja miradi iliyojengwa na Dk. Mwakyembe kuwa ni pamoja na barabara ya Kikusya-Matema na ya kwenda Bandari ya Itungi na mipango miradi mingine ambayo alikuwa amepanga kuifanya ambayo CHADEMA ikishika jimbo hilo itaiendeleza.

Mgombea huyo akizungumza juzi kwenye mkutano uliofanyika Kyela Mjini, alisema huwezi ukawa unaomba ridhaa ya kuwatumikia wananchi halafu hujengi misingi iliyoanzishwa na mtangulizi wako.

"Kiongozi unapoingia madarakani ni lazima ujue nini kilifanywa na aliyekuwapo ili nawe uweze ' ku-push' yale ambayo yalikuwa hayajakamilika," alisema.

Akizungumzia kuhusu tatizo la maji, alisema wananchi wakimchagua atahakikisha anajenga mradi mkubwa kwa kutoa maji Ziwa Nyasa au katika mito inayoizunguka Wilaya ya Kyela.

Kuhusu soko la Kyela mjini alisema atahakikisha linarejeshwa kwa wananchi, tofauti na sasa shughuli za ukusanyaji ushuru Chama Cha Mapinduzi (CCM) ndicho kimepewa zabuni.

## Abanwa utekelezaji ahadi akichaguliwa

**Na Beatrice Moses,** TUDARCO

MGOMBEA udiwani wa Kata ya Saranga, Edward Laizer ametakiwa kuiga nyayo za mgombea urais wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), John Magufuli za kutimiza ahadi zake kwa wananchi.

Laizer, anayegombea nafasi hiyo kwa tiketi ya CCM, alikumbana na darasa hilo juzi wakati akiwa kwenye kampeni yake ya shina kwa shina katika Mtaa wa Saranga, wakati wa harakati za kusaka kupigiwa kura za ushindi.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, baadhi ya wakazi hao walisema utekelezaji wa ahadi aliofanya Rais Magufuli ikiwamo kukomesha kero ya upatikanaji wa majisafi na salama katika eneo hilo, unawawashawishi kumpigia kura tena ili ashike nafasi hiyo. Zaina Hassan, mkazi wa shina namba nane, linaloongozwa na Mjumbe Amina Salum, alimtaka mgombea huyo kuonyesha tofauti yake na wagombea wengine waliowahi kupita kuomba kura na baada ya kushinda hawakutimiza ahadi zao, hivyo kusababisha waendelee kuishi kwenye changamoto ikiwamo ya ukosefu wa miundombinu hasa barabara na kutokuwa na zahanati.

"Ahadi zako ni nzuri kama zitatekelezwa, lakini wapo wenzako waliokutangulia waliwahi kuahidi kama hivi, lakini baada ya ushindi hawakuonekana, sasa wewe utatutekelezeaje? Alihoji Zaina.

Akijibu swali hilo, mgombea huyo alisema anahofu ya Mungu na kuwa amekuwa akiwatumikia wakazi wa eneo hilo wenye uhitaji wakiwamo yatima na wajane, amepokea baraka, hivyo ameamua kujitokeza kugombea nafasi hiyo akiwa na kiu ya kuhakikisha anashiriki kutatua matatizo yanayowakabili wakazi wa Saranga.

"Sikujitokeza kugombea nafasi hii ili kusaka fedha ya kumnunulia mke wangu kitenge, nashukuru Mungu ameniwezesha kumudu kumnunulia mke wangu vitenge tangu nilipoamua kuwahudumia kwa bidii yatima na wajane, sasa nataka nishiriki kuongoza kata ili niweke alama nzuri zaidi," alisema Laizer. Alisema ameamua kufanya kampeni kwa mtindo huo ikiwa ni hatua yake ya kubaini maeneo yenye changamoto ili kupanga namna nzuri ya kutatua, atakaposhinda katika kinyang'anyiro hicho na kuwa diwani. Alitaja matatizo ambayo yamebainika kuwapo katika eneo hilo baadhi ni pamoja na kutokuwa na eneo la soko, vijana na kinamama kukosa mikopo ya masharti nafuu na kukosekana kwa kituo cha polisi.

Awali, Mratibu wa kampeni ya mgombea huyo Seif Kibangu, aliwaeleza wakazi wa mashina namba nane na 11 kuwa amemshawishi Laizer kupita kwa miguu badala ya kutumia gari ili ajionee maeneo yenye ubovu wa barabara na changamoto nyingine hivyo iweze kuwa kichocheo chake cha kutekeleza ahadi baada ya kuchaguliwa na kushinda nafasi hiyo.

Kwa upande wake Mjumbe wa shina namba 11, Pascal Kaghembe, aliwashukuru wananchi waliojitokeza kumsikiliza mgombea huyo na kuwasihi wajitokeze kwa wingi siku ya kupiga kura.

HABARI KITAIFA

# Miradi ya maendeleo GGML, serikali yawakuna viongozi dini

**Na Mwandishi Wetu**

VIONGOZI wa dini mbalimbali mkoani Geita wamefanya ziara ya kukagua miradi ya maendeleo inayotekelezwa mkoani humo na kueleza kufurahishwa na usimamizi thabiti wa miradi hiyo kwa maendeleo ya Tanzania.

Viongozi hao wamefanya ziara hiyo ambayo imedhaminiwa na Kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML) pamoja na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Geita kwa lengo la kuona na kupata ufafanuzi wa miradi inayotekelezwa mkoani humo.

Akizungumzia ziara hiyo iliyofanywa jana, Mkuu wa Mkoa wa Geita, Mhandisi Robert Gabriel, alisema ofisi yake inatambua mchango mkubwa wa viongozi wa dini katika kutunza amani na umoja ndani ya jamii.

"Huwezi kupata maendeleo katika jamii yoyote bila kuwa na amani. Amani inayotupatia maendeleo katika nchi yetu na mkoa wetu wa Geita inalindwa na viongozi wa dini ambao siku zote wamekuwa na ushawishi kwa waumini wao kuhubiri amani," alisema.

Aidha, Meneja Miradi inayofadhiliwa na Geita Gold Mining Limited (GGML) kupitia fedha za Wajibu wa Kampuni kwa Jamii (CSR), Moses Rusasa, alisema katika ziara hiyo kuwa lengo la GGML ni kuhakikisha jamii inayozunguka mgodi inafaidika.

"Tunatekeleza miradi mingi ndani ya mkoa wa Geita kwa sababu mojawapo ya tunu inayoongoza Kampuni ya GGML ni kufaidisha jamii inayotuzunguka. Katika ziara hii na viongozi wa dini, tumetembelea soko la dhahabu, Soko la Katundu pamoja na kituo cha uwekezaji (EPZA) miradi ambayo imefadhiliwa na Kampuni ya GGML kwa maendeleo ya watu wa Geita," alisema Rusasa.

Akitoa neno la shukrani wakati wa ziara hiyo, Mwenyekiti wa Umoja wa Dini mkoani Geita, Askofu Stephano Saguda, alimshukuru Mkuu wa Mkoa wa Geita kwa kuwatembeza katika ziara hiyo na kumpongeza kwa kazi nzuri ya kusimamia maendeleo katika Mkoa wa Geita.

"Tunampongeza sana Rais wa John Magufuli kwa kuupatia Mkoa wa Geita kiongozi makini anayesimamia maendeleo. Nawapongeza pia Kampuni ya GGML kwa kushirikiana vyema na serikali hususani Halmashauri za Geita na kutekeleza miradi mikubwa yenye gharama kubwa katika Mkoa wa Geita," alisema Askofu Saguda.

Kwa miaka 10 iliyopita, GGML imewekeza jumla ya Dola milioni 25 kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo mkoani Geita na Tanzania kwa ujumla. Mkakati ni kutenga pia Dola milioni 53 kwa ajili ya miaka 14 ijayo.



Mkuu wa Mkoa wa Geita, Mhandisi Robert Gabriel (katikati), akiwaelezea viongozi wa dini mkoani Geita mradi wa soko la dhahabu pamoja na vyumba vya biashara vilivyofadhiliwa na GGML kwa ushirikiano na Halmashauri ya Mji wa Geita. **MPIGAPICHA WETU**

# TAHOSA yajivunia kuinua ufaulu Simiyu

**Na Happy Severine,** SIMIYU

UMOJA wa Wakuu wa Shule za Sekondari za Umma na Binafsi Tanzania (TAHOSA) mkoani Simiyu, umesema unajivunia kuinua kiwango cha ufaulu wa wanafunzi na kuingia katika kumi bora katika mitihani ya kitaifa katika kidato cha pili, nne na sita katika matokeo ya mwaka 2019.

Kiwango hicho cha ufaulu kimeelezwa kuinuliwa kutokana na usimamizi wa ufuatiliaji kabambe wa taaluma shuleni uliotokana na nidhamu ya walimu na wanafunzi shuleni.

Hayo yalibainishwa jana na Mwenyekiti wa TAHOSA Mkoa wa Simiyu, Amede Ndoje, wakati akisoma taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya umoja huo katika kikao chao kilichofanyika katika mjini Bariadi.

Alisema umoja huo umekuwa na msaada mkubwa katika kuhakikisha unasimamia mikakati inayowekwa ya kuinua elimu.

Ndoje aliongeza kuwa mbali na changamoto wanazokutana nazo, lakini kwa kiasi kikubwa wameweza kufikia malengo yao wanayojiwekea kila mwaka.

Awali akizungumza katika kikao hicho Ofisa Elimu Mkoa, Ernest Hinju, alisema mkoa wa Simiyu umebahatika kuwa na wakuu wa shule wenye bidii katika kazi, ushirikiano na umoja wa kuleta mabadiliko.

Hinju alisema kuwa mafanikio yote ambayo yanapatikana katika sekta hiyo yanatokana na viongozi hao kuwa na ushirikianao na viongozi mbalimbali ikiwamo kufuata maelekezo ya viongozi wa mkoa na wilaya.

Akifungua mkutano huo Katibu Tawala wa Mkoa, Miriam Mmbaga, aliwataka viongozi hao kuendelea kutekeleza mikakati yote 12 ambayo wamejiwekea kwenye sekta hiyo, ili kuendelea kufanya vizuri.

## Sera yaandaliwa kuwalinda watoto

**Na Yasmine Protace,**
MKURANGA

UONGOZI wa Shule ya Sekondari ya Ujenzi iliyoko Wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani, umeandaa sera ya kuwalinda watoto kwa kuzijua haki zao wakiwa ndani au nje ya shule.

Hayo yalibainishwa na mkurugenzi mtendaji wa shule hiyo, Peter Mutembei, katika mahafari ya 19 ya kidato cha nne ya shule hiyo.

"Tumeandaa sera katika shule yetu ya kumlinda mtoto kwa kuzijua haki zake akiwapo nyumbani au shuleni," alisema mkurugenzi huyo.

Aliongeza kuwa hata kama haki za mtoto zimekiukwa nyumbani na taarifa wakazipata wahusika watachukuliwa hatua.

Akizungumzia maendeleo ya taaluma kwa wanafunzi wa shule hiyo, Mutembei alisema kuwa shule yao imekuwa ikifanya vizuri katika mitihani ya kidato cha pili na kidato cha nne ni kwa sababu ya kutoa motisha kwa walimu na wanafunzi ikiwamo na ushirikiano mzuri uliopo kati ya walimu na wanafunzi.

Mkuu wa shule hiyo, Josia Philipo, alisema kuwa shule yao imejiwekea mikakati mbalimbali ambayo itachangia kukuza elimu ambayo inatolewa katika shule hiyo.

Aliitaja baadhi ya mikakati ni kuwa pamoja na kuwa na wafanyakazi wa kutosha, kuhakikisha huduma zote zinazotakiwa kuwapo shule kuhakikisha zipo kwa ajili ya kuwawezesha walimu kufanya kazi vizuri.

Akizungumzia mafanikio kitaaluma alisema kuwa katika kipindi cha miaka mitatu kwa, matokeo ya kidato cha nne shule ilifaulu vizuri mitihani ya kidato cha nne ambapo ufaulu ulikuwa wa asilimia 100.

Mkuu huyo wa shule aliwataka wahitimu hao kuendelea kuwa na maadili mema, na kuwaeleza kuwa elimu pekee ndio mtaji wa maisha.

Ofisa Elimu ya Sekondari Wilaya ya Mkuranga, Benjamini Majoya, alisema kuwa elimu ya kidato cha nne sio mwisho wa elimu.

Majoya alisema Wilaya ya Mkuranga inatambua mchango wa shule hiyo, na kuahidi kuendelea kushirikiana nayo kwa ajili ya maendeleo ya elimu.

## Wazawa wataka zabuni serikalini

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAWEKEZAJI wa viwanda vya ndani wilayani Kahama mkoani Shinyanga wameiomba serikali kuwapatia zabuni ya kusambaza vifaa vya ujenzi katika majengo yanayojengwa na serikali.

Wametaka zabinu hizo hasa katika sekta ya elimu, afya na miundombinu ya maji ili kupata soko la uhakika la bidhaa zinazozalishwa nchini.

Walitoa ombi hilo juzi wakati wa uzinduzi wa Maonyesho ya Mkopo wa vyumba na vifaa vya ujenzi yaliyofanyika katika viwanja vya Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) kwa ufadhili wa NMB Tawi la Kahama na kuhudhuliwa na wafanyabiashara wa vifaa vya ujenzi mjini hapa.

Range Chacha, mmoja wa wawekezaji Mjini hapa, alisema wamekuwa wakizalisha bidhaa mbalimbali kupitia viwanda vyao, lakini wamekuwa wakikosa masoko ya uhakika ya kuuza bidhaa zao na kusababisha wengi wao kusitisha uzalishaji mpaka pale atakapopata tenda kutoka kwa makandarasi.

Alisema kuwa, ili kumsaidia mwekezaji wa ndani, serikali inatakiwa kuhakikisha inatoa tenda kwa wawekezaji wa ndani ikiwa ni pamoja na kuwahimiza makandarasi wanaopata tenda katika majengo ya serikali kuhakikisha wanatumia bidhaa zinazotoka kwenye viwanda vya ndani na sio kutoka nje.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, alisema Benki ya NMB ni washirika wakubwa wa serikali katika shughuli mbalimbali za kimaendeleo ambazo ndizo zionazosababisha kujenga uchumi wa nchini.

Macha alizitaka Halmashauri za Msalala, Ushetu na Kahama Mjini, kuhakikisha wananunua bidhaa za ujenzi zinazotengenezwa katika viwanda vya Mkoa wa Shinyanga kwani bidhaa zinazotengenezwa ni nzuri na zinakidhi viwango kama zile za kutoka nje tuu.

# Serikali yafanya uwekezaji mkubwa matibabu saratani

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imesema maboresho yaliyofanyika kwenye sekta ya afya katika kipindi cha kwanza cha miaka mitano ya uongozi wa Rais John Magufuli yameleta neema kubwa katika masuala ya tiba ikiwamo kupunguza gharama za kuwatibu wagonjwa wa saratani nje ya nchi.

Hayo yalibainishwa Jumamosi na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, jijini Dar es Salaam wakati wa kuhitimisha mbio za NMB Bima Marathon 2020.

Majaliwa aliipongeza Benki ya NMB na wadau wengine kwa ushiriki wao katika juhudi za taifa kupambana na magonjwa yasiyoambukizwa, ambayo alisema yamekuwa ni chachu kubwa ya kuongeza gharama za matibabu nchini.

Aliwaeleza washiriki kuwa saratani na magonjwa mengine yasiyoambukizwa ni mzigo mkubwa kiuchumi duniani na kikwazo cha maendeleo kutokana na gharama za kuyatibu ni mabilioni ya dola za Kimarekani kwa mwaka.

Majaliwa alisema taarifa ya Shirika la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) ya mwaka 2013 inaonyesha kuwa katika kipindi cha miaka 20 gharama hizo zingeongezeka na kufikia dola 47 trilioni. Alisema ni kiasi cha fedha ambacho kingeweza kupunguza umaskini kwa watu bilioni 2.5 duniani katika kipindi cha miaka 50. "Nawashukuru NMB kwa kuja na wazo hili la NMB Bima Marathon ili kuhamasisha pia kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa mazoezi kama njia sahihi ya kuweka miili sawa dhidi ya magonjwa kama saratani," alisema.

"Kadhalika nitoe wito kwa sekta binafsi kushirikiana na serikali katika kuhamasisha matumizi ya bima dhidi ya majanga mbalimbali yakiwamo magonjwa ya kuambukiza kama saratani," pia alisema kisha kukabidhi hundi ya Sh.milioni 100 zilizokusanywa na benki hiyo kupitia mbio za kilomita tano kwa ajili ya watoto wanaotibiwa saratani katika Hospitali ya Taifa Muhimbili.

Kwa mujibu wa Waziri Mkuu Majaliwa, mwitikio wa Watanzania kwenye suala la huduma za bima bado ni mdogo na hii imekuwa ni changamoto kubwa si tu kwa maendeleo ya nchi, lakini katika kukabiliana na vitu kama gharama kubwa za matibabu.

Mwenyekiti wa bodi ya benki hiyo, Dk. Edwin Mhede, alisema wako tayari kupitia mapato yake halali na mfano mzuri wa mchango wake ni kusaidia kukusanya Sh. milioni 100 kwa ajili ya matibabu ya watoto wenye magonjwa ya saratani.

Naye Ofisa Mtendaji Mkuu wa benki hiyo, Ruth Zaipuna, alisema uamuzi wa kuihamasisha jamii kuchangia matibabu ya watoto wenye saratani kupitia mbio za hisani za NMB Bima Marathon ulitokana na mwezi Septemba kuwa maalum kwa uhamasishaji wa kuongeza uelewa kuhusu magonjwa ya saratani kwa watoto duniani.

Alisema mbio hizo zimeleta mwamko mpya na uelewa mkubwa kuhusu bima mbalimbali nchini na pia zimeipa fursa jamii kushiriki katika mazoezi ili kujenga miili na kupunguza maradhi ambayo yanazuilika kwa njia ya mazoezi.




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (kulia), Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa benki hiyo, Dk. Edwin Mhede, wakimkabidhi mfano wa hundi ya Sh. milioni 100 Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Prof. Lawrence Museru (kushoto), kwa ajili ya kusaidia watoto wenye saratani wakati wa mbio za hisani za NMB Bima Marathon zilizofanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Wa pili kushoto ni Mtendaji Mkuu wa Sanlam Afrika Mashariki, Julius Magambe. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanafunzi Tanzania kuwakilisha Afrika mashindano ya TEHAMA

**Na Mwandishi Wetu**

WANAFUNZI wa Tanzania ni miongoni mwa washiriki wa fainali za mashindano ya kimataifa ya TEHAMA kwa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Mashindano hayo yanayoandaliwa na Huawei, kaulimbiu yake ni "Connectivity, Glory, Future", ambapo kwa mwaka jana wanafunzi kutoka Tanzania na Nigeria walikuwa washindi wa jumla katika shindano hilo, hivyo kuwakilisha ukanda huo katika mashindano ya dunia.

Shindano hilo lilizinduliwa jijini Johannesburg, Afrika Septemba 10, mwaka huu kwa njia ya mtandao. Shindano hilo linaaminika kuwa ndiyo kubwa zaidi barani Afrika kwa kushirikisha nchi 14 na kuhusisha wanafunzi zaidi ya 50,000.

Shindano la TEHAMA linaloandaliwa na Huawei, kwa mwaka huu limeshirikisha zaidi ya nchi 70 ulimwenguni, na kushindanisha wanafunzi 150,000 kutoka vyuo zaidi ya 2,000. Tangu kuzinduliwa kwake miaka mitano iliyopita, shindano la TEHAMA la Huawei limeendelea kukua na kuwa shindano kubwa zaidi la TEHAMA barani Afrika.

Katika uzinduzi uliohudhuriwa na wadau mbalimbali wa sekta ya mawasiliano, UNESCO na wanafunzi, Makamu Rais wa Huawei Afrika Kusini, Liao Yong, alielezea umuhimu wa mawasiliano katika zama hizi za kutokusogeleana.

"Utofauti katika mapokeo ya kidigitali unazidi kuongezeka katika kipindi hiki ambacho dunia imekumbwa na janga la Covid-19. Wakati watu wanapojisomea na kufanya kazi mtandaoni, wale wenye changamoto za kidigitali wanaathirika zaidi," alisema Liao.

Katika semina ya mtandaoni iliyoandaliwa na UNESCO hivi karibuni, ilibainishwa kuwa miundombinu ya kidigitali ni miongoni mwa changamoto kubwa zinazoikabili sekta ya elimu ya juu barani Afrika. "Kufanya shindano hili la TEHAMA mtandaoni kwa kipindi hiki kuna thamani ya kipekee, inaonyesha kwamba Huawei kama waasisi wa miundombinu ya kidigitali Afrika pia tuko makini sana na mkakati wetu wa kuwekeza kwenye vipaji. Mkakati unajumuisha mambo matatu; kuwafundisha wataalamu wa TEHAMA kidigitali, kuhamasisha na kuwawezesha wanafunzi wa TEHAMA na kuongeza uelewa kwa watu wa kawaida.

Kampuni ya Huawei imewekeza zaidi katika kujiandaa na mashindano hayo kwa kufanya maonyesho kwenye vyuo 300, katika nchi 14 za Kusini mwa Jangwa la Sahara, na jumla ya wanafunzi 50,000 watashiriki. Mafunzo kuhusu mashindano haya yamesaidia zaidi ya wanafunzi 300 kupata ofa za kazi.


Aidha, mafunzo haya yamekuwa na umuhimu mkubwa kwa wanafunzi. mwanafunzi wa TEHAMA wa Tanzania, Emanuel Chaula, alifurahi kwamba timu ya wanafunzi wa Tanzania ilikuwa moja ya timu kutoka nchi mbili zilizoshinda katika mashindano ya mwaka jana.

"Tulifanya kazi kwa bidii kama timu kwa sababu tulitaka kutumia fursa hiyo kusafiri kwenda China kushindana katika fainali za ulimwengu mzima. Tulitaka kuonyesha Afrika na ulimwengu kuwa Tanzania ni mdau mkubwa wa TEHAMA na tunataka kuwa sehemu ya ukuaji huo katika nchi yetu," alisema.

Nipashe
Spotika



WACHEZAJI 10 WENYE KASI ZAIDI EPL UK. 12&13



# NYOTA WA5 WANAOMKUBALI RONALDO KULIKO MESSI

**LONDON, England**

MWEKAJI rekodi wa timu ya Taifa ya Ureno, Cristiano Ronaldo alilipamba jina lake kwenye vitabu vya historia baada ya kufunga bao lake la 100 na 101 kwenye mechi za kimataifa, Jumanne iliyopita.

Ronaldo kwa sasa akiwa anacheza kule Juventus bila shaka yoyote ni mmoja wa wachezaji bora zaidi kuwahi kushuhudiwa kwenye mchezo wa soka duniani.

Jumanne usiku, Ronaldo aliweka historia hiyo kwa mara nyingine tena kwa rekodi ambayo inaweza kukaa kwa miaka mingi.

Mchezaji huyo wa zamani wa Real Madrid alifunga bao la 100 na 101 kwa timu ya Taifa ya Ureno wakati ikiibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Sweden kwenye Ligi ya Mataifa ya UEFA.

Na hilo likamfanya kuwa mchezaji wa kwanza barani Ulaya kufikisha idadi hiyo ya mabao kwa timu yake ya taifa. Ronaldo alihitaji mechi 165 tu kufikisha rekodi hiyo.

Amepitwa mabao nane tu ili kufikia rekodi ya kufunga mabao mengi ya kimataifa, ambapo kwa sasa rekodi hiyo inashikiliwa na mchezaji wa zamani wa Iran, Ali Daei, ambaye ana mabao 109 aliyoifungia nchi yake.

Rekodi hiyo ni moja kati ya rekodi nyingi alizoziweka Ronaldo, ambaye ni mmoja wa wachezaji bora wa kizazi hiki pamoja na nahodha wa Barcelona, Lionel Messi.

Wawili hao kwa pamoja wameshinda mara 11 tuzo ya Ballon d'Or tangu waanze kucheza soka.

Wanasoka wengi mara kwa mara wamekuwa wakiulizwa kuhusu nani ni bora zaidi kati ya wawili hao.

Makala haya yanakuchambulia wanasoka nyota watano ambao wamemchagua Ronaldo kuwa bora zaidi ya Messi, twende sasa...

**#5. Gini Wijnaldum | Liverpool**

Kiwango cha Gini Wijnaldum kimeimarika kwa kipindi cha miaka michache ya hivi karibuni. Raia huyo wa Uholanzi amekuwa kwenye nafasi nzuri katika safu ya kiungo mshambuliaji chini ya kocha, Jurgen Klopp. Wijnaldum ambaye alikuwa nguzo muhimu kwa 'Wekundu' hao alifunga mabao mawili wakati Liverpool ikiitoa Barcelona hatua ya nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 29, aliulizwa kumchagua kati ya Messi na Ronaldo katika matukio kadhaa. Katika tukio la kwanza alijibu kidiplomasia kwa kusema;

"Muda mwingine nasema Lionel Messi, wakati mwingine nasema Cristiano Ronaldo. Si haki kuchagua mmoja kati yao, kwa sababu alichonacho mchezaji mmoja, mwingine hana. Kwa upande wangu wote ni wachezaji bora duniani."

Hata hivyo, katika mahojiano ya 'lazima ujibu', Wijnaldum aliulizwa kuchagua mmoja kati ya Messi na Ronaldo. Na raia huyo wa Uholanzi alimchagua Ronaldo.

Hivi sasa Wijnaldum amekuwa akihusishwa sana kuhamia kule Barcelona usajili ambao unatajwa unaweza kufanyika katika wiki chache zijazo.

**#4 Michael Owen | Nyota wa zamani Liverpool, Manchester United, Real Madrid**

Mchezaji mwingine kwenye orodha hii ni gwiji wa zamani wa mabingwa wa Ligi Kuu ya England, Liverpool, Michael Owen ambaye amemchagua Ronaldo juu ya Messi. Owen mwenye umri wa miaka 40, kwa sasa alikuwa mchezaji wa mwisho wa Uingereza kushinda Ballon d'Or, tuzo ambayo Ronaldo ameitwaa mara tano hadi sasa.

Owen alielezea kwa nini amemchagua Ronaldo juu ya Messi. Muingereza huyo alisema;

"Kufunga mabao ni kazi ngumu kwenye soka na (Ronaldo) ameifanya kuwa rahisi. Anafunga kwa kichwa, mguu wa kushoto au kwa mguu wa kulia. Messi ni mchezaji mzuri sana, lakini ukiangalia kwa takwimu ya wawili hao Messi na Ronaldo, unatakiwa kumchagua Ronaldo kwa sababu ana vitu vingi tofauti."

Akaendelea kusema, "Pengine Ronaldo ndio mchezaji mwenye kasi zaidi akitumia mguu wa kulia na kushoto pamoja na kichwa. Nafikiri Messi amezidiwa na Ronaldo kwa mbinu."

**#3. Ruud van Nistelrooy | Nyota wa zamani Manchester United, Real Madrid**

Katika orodha hii, Ruud van Nistelrooy ndiye mchezaji pekee aliyecheza na Cristiano Ronaldo katika timu moja. Gwiji huyo wa Uholanzi anabaki kama mmoja wa mshambuliaji bora zaidi wa kati kwa Manchester United, akiwa amefunga mabao 150 katika mechi 219 alizowachezea 'Mashetani Wekundu' hao.

Van Nistelrooy na Ronaldo walikuwa haziivi wakati wakicheza pamoja pale Old Trafford. Hata hivyo, licha ya tofauti zao hizo uwanjani, Van Nistelrooy alimchagua Ronaldo kuwa bora zaidi ya Messi.

Mchezaji huyo wa zamani wa Real Madrid, aliyecheza kwa misimu mitatu akiwa na Ronaldo pale Old Trafford, Van Nistelrooy, amesema:

"Hakuwa mjinga. Mara zote alikuwa tayari kupokea ushauri. Alikuwa mtu mzuri kwenye vyumba vya kubadilishia nguo."

**#2 Kylian Mbappe | Paris Saint-Germain**

Huyu ni mmoja wa mashabiki wakubwa kwa Ronaldo, kwani wakati akikua Kylian Mbappe alikuwa akipenda zaidi kumwangalia nyota huyo wa Ureno. Nyota huyo wa Ufaransa anatajwa kwamba ndiye atakuwa mchezaji bora zaidi duniani baada ya kumalizika kwa zama za Messi na Ronaldo.

Akizungumza kuhusu nani bora ambaye atamchagua kati ya Messi na Ronaldo, Mbappe alibainisha;

"Kutoka mwaka mmoja hadi mwingine, chaguo langu linabadilika kati ya Cristiano Ronaldo na Lionel Messi, ingawa naweza kukubali kwamba nimemchagua zaidi Ronaldo. Nilimpenda wakati nikiwa mdogo."

Mbappe amezungumza kuvutiwa na nyota huyo wa Juventus katika matukio kadhaa. Mfaransa huyo amebainisha kwamba wachezaji ambao walikuwa wanamvutia wakati akikua ni Zinedine Zidane na Cristiano Ronaldo.

Nyota hyo mwenye umri wa miaka 21, ambaye alichomoza Ulaya akitokea kule AS Monaco, alibainisha kwamba chumbani kwake aliweka picha nyingi sana za Ronaldo kwenye ukuta.

Mshindi huyo wa Kombe la Dunia anachukuliwa kama mmoja wa wachezaji wanaowaniwa sana na Real Madrid. Kama atahamia kwa miamba hao wa Hispania atakuwa amefuata nyao za Ronaldo na Zidane.

**#1. Pele | Nyota wa zamani Santos**

Pele anatajwa kama ndio mchezaji bora wa wakati wote na mara zote amekuwa wazi kumchagua Ronaldo kama mchezaji bora na amekuwa akimfananisha na yeye wakati akicheza.

Ingawa gwiji huyo wa zamani wa timu ya Taifa ya Brazil anatambua ubora wa Messi, lakini Pele anaamini Ronaldo ndiye mchezaji bora zaidi duniani kwa sasa. Nyota huyo wa zamani wa Santos amesema kutoshuka kwa kiwango cha Ronaldo ndio kunamfanya kuwa bora zaidi ya Messi.

Akizungumza na chaneli ya YouTube kupitia Daily Mail kuhusu nyota hao wawili, Machi mwaka huu, Pele mwenye umri wa miaka 79, alieleza:

"Leo hii mchezaji bora duniani ni Cristiano Ronaldo. Nafikiri yeye ni bora kwa sababu ya kutoshuka kiwango chake, lakini huwezi kumsahau (Lionel) Messi, lakini yeye si straika."

Pele ana rekodi ya kubeba Kombe la Dunia mara tatu na ni mmoja wa wachezaji waliofunga mabao mengi zaidi kipindi akiwa mchezaji.

## ISIKUPITE

MOHAMED Salah amekuwa mchezaji wa kwanza Liverpool kuweza kuweka rekodi ya kufunga hat-trick katika mechi ya fungua msimu Ligi Kuu England kwa klabu hiyo tangu John Aldridge, alipofanya hivyo miaka 32 iliyopita katika msimu wa 1988-89. Salah alifunga hat-trick hiyo juzi wakati wakishinda 4-3 nyumbani dhidi ya Leeds United.



## Extra Time

# WACHEZAJI 10 WENYE KASI ZAIDI EPL


Walker

**LONDON, England**

LIGI Kuu England ni maarufu kwa kasi na kutumia nguvu. Baadhi ya wachezaji wenye kasi zaidi duniani wanacheza soka kwenye ligi hiyo.

Ligi Kuu ya soka ya England ndio ligi ya soka tajiri duniani na pia inajulikana kwa staili yake ya kutumia nguvu. Ndio maana Ligi ya England imekuwa moja ya ligi ngumu sana duniani. Wachezaji wengi kwenye ligi hiyo wana kasi kubwa ya kukimbia kama wanariadha wa mbio za mita 100.

Makala haya yanawachambua wachezaji 10 wenye kasi zaidi kwenye Ligi Kuu England, wafahamu sasa...

**#10. Phil Foden (Manchester City)**

Phil Foden mwenye umri wa miaka 20, alianza kucheza soka la kulipwa pale Manchester City kipindi cha majira ya joto mwaka 2016, lakini jina lake lilipaa zaidi msimu uliopita wakati alipofunga mabao nane katika mechi 38 alizocheza kwenye mashindano yote.

Kiungo huyo anayetumia mguu wa kushoto anatambulika kwa uwezo wake wa kucheza katika winga zote au kiungo. Foden, ndio anachukuliwa kama mrithi wa gwiji, David Silva.

**#9. Fred (Manchester United)**

Raia huyo wa Brazil, Fred alitua kwenye Ligi Kuu ya England kipindi cha majira ya joto mwaka 2018. Manchester United ilipata huduma ya mshindi huyo mara tatu wa taji la Ligi Kuu ya Ukraine kutoka kwa Shakhtar Donetsk ili kuimarisha safu yao ya kiungo.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 27, alicheza mechi 48 katika mashindano yote msimu uliopita na mara nyingi akicheza nafasi ya kiungo wa kati.

**#8. Shane Long (Southampton)**

Shane Long wa Southampton ni mkongwe kwenye Ligi Kuu ya England, akiwa amecheza zaidi ya mechi 300 kwenye mashindano yote katika klabu tatu tofauti.

Hata hivyo, imekuwa ngumu kupata mabao kwa straika huyo wa kimataifa wa Ireland ambaye amecheza katika klabu 13 tofauti kwenye ligi, lakini alifunga mabao 10 kwa msimu mmoja tu.

**#7. Ainsley-Maitland Niles (Arsenal)**

Ainsley-Maitland Niles amefunga mara moja tu katika mechi 53 za Ligi Kuu alizoichezea Arsenal katika misimu mitano tofauti.

Muingereza huyo, ambaye alikuwa anacheza katika safu ya ulinzi chini ya Unai Emery, anapenda zaidi kucheza nafasi ya kiungo. Hata hivyo, Maitland Niles anajulikana kwa kasi na spidi yake uwanjani.

**#6. Caglar Soyuncu (Leicester City)**

Caglar Soyuncu aliwasili kwenye Ligi Kuu ya England akiichezea Leicester City kipindi cha majira ya joto mwaka 2018 baada ya misimu miwili katika klabu ya Freiburg kwenye Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga.

Raia huyo wa Uturuki alikuwa nguzo kubwa kwa Leicester City msimu uliopita wakati walipokosa kidogo tu kupata nafasi ya kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya kufungwa na Manchester United siku ya mwisho ya msimu.

**#5. Aaron Wan-Bissaka (Manchester United)**

Baada ya kuanza kucheza soka la kulipwa akiwa na Crystal Palace, ambako alionyesha kiwango cha kuvutia, Aaron Wan-Bissaka aliwasili Manchester United mwanzoni mwa msimu uliopita.

Mlinzi huyo wa kulia mwenye umri wa miaka 22, amekuwa nguzo kubwa sana kwa safu ya ulinzi ya Manchester United wakati ikimalliza nafasi ya tatu msimu uliopita.

**#4. Trezeguet (Aston Villa)**

Mahmoud Ahmed Ibrahim Hassan, anajulikana zaidi kama Trezeguet kwa uwezo wake wa kufunga akilinganishwa na straika wa zamani wa Ufaransa, David Trezeguet, aliwasili kwenye Ligi Kuu ya England kipindi cha majira ya joto mwaka 2019.

Trezeguet ambaye alicheza nchini Misri, Ubelgiji na Uturuki, alikuwa mchezaji muhimu kwa Aston Villa msimu uliopita baada ya kuinusuru kutoshuka daraja.

**#3. Mason Greenwood (Manchester United)**

Mason Greenwood mwenye umri wa miaka 18, alianza kucheza kwenye Ligi Kuu ya England akiwa na Manchester United mwaka 2018.

Greenwood anayetumia miguu yote miwili, anajulikana kwa kasi na nguvu akiwa anacheza nafasi ya winga kabla ya kuhamishiwa kukipiga kama mshambuliaji wa kati.

**#2. Adama Traore (Wolverhampton Wanderers)**

Winga huyu mwenye umri wa miaka 24 raia wa Hispania, Adama Traore aliwasili kwenye Ligi Kuu England kipindi cha majira ya joto mwaka 2015 wakati alipojiunga na Aston Villa, lakini alipotua Wolverhampton Wanderers ndiko alikoonyesha zaidi kipaji chake na kung'ara.

Traore, ambaye analinganishwa na Messi na Ronaldo na kocha wake wa zamani kule Villa, Tim Sherwood, anajulikana kwa staili yake ya mbio nyingi na nguvu ya kumiliki mpira.

**#1. Kyle Walker (Manchester City)**

Mlinzi wa kulia wa zamani wa Tottenham Hotspur, Kyle Walker, ambaye kwa sasa anacheza kule Manchester City, ni mkongwe kwenye Ligi Kuu ya England, akiwa amecheza misimu 13.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 30, anajulikana kwa kucheza kwa nguvu, kasi na ni mchezaji ambaye amekamilika na amekuwa nguzo muhimu kwa kocha Pep Guardiola pale City baada ya kuondoka kule Spurs kipindi cha majira ya joto mwaka 2017.

## Nukuu


"Kwa kiasi fulani nina hasira juu yangu kwa sababu nimekosa nafasi nyingi za kufunga, msimu huu nataka kuwa na makali zaidi kwenye goli kuliko msimu uliopita. Kwani nataka kufunga na kufunga kila nikipata nafasi," **mshambuliaji wa Tottenham Hotspur, Son Heung.**



"[Kalidou] Koulibaly ana bei yake iliyowekwa na kama klabu itashindwa kuifikia, hataweza kuondoka, **"Kocha Mkuu wa Napoli, Gennaro Gattuso akitoa msimamo wake kuhusu Koulibaly ambaye anawindwa na Manchester City.**



"Kusema kwa heri mara zote ni kitu kigumu, naondoka sehemu ambayo niliona kama nyumbani kwangu," **Arthur Melo akiaga Barcelona kabla ya kutua Juventus.**



# REKODI 5 KALI LIGI KUU BARA 2020/21 IKIANZA

Na Adam Fungamwango

MSIMU wa Ligi Kuu Tanzania Bara 2020/21, ulianza Septemba 6 kwenye viwanja mbalimbali nchini na kutengeneza rekodi tofauti tofauti kwa timu na wachezaji.

Raundi ya kwanza ilianza kwa mechi tisa, Namungo ilishinda nyumbani bao 1-0 dhidi ya Coastal Union, Biashara ikiifunga Gwambina bao 1-0, Dodoma Jiji nayo ikishinda 1-0 dhidi ya Mwadui, Ihefu ikifungwa mabao 2-1 dhidi ya Simba, Mtibwa Sugar ikitoa suhulu na Ruvu Shooting, Yanga ikitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Tanzania Prisons, KMC ikiifumua Mbeya City mabao 4-0, JKT Tanzania ikishinda 1-0 dhidi ya Kagera Sugar na Azam ikishinda bao 1-0 dhidi ya Polisi Tanzania.

Raundi ya pili ilianza Ijumaa iliyopita, Gwambina ikitoka suluhu na Kagera Sugar, Azam ikiichapa Coastal mabao 2-0, na Jumamosi JKT Tanzania ikifumuliwa mabao 2-0 dhidi ya Dodoma Jiji, KMC ikiendeleza kipigo cha mabao 2-1 dhidi ya Prisons, Simba ikitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Mtibwa Sugar.

Zifuatazo ni rekodi zilizowekwa na kuvunjwa kwenye baadhi ya mechi, pamoja timu na wachezaji waliziweka na kuzivunja pia, tiririka zazo...

**#1. Bigirimana Blaise (Namungo FC)**

Straika huyu ameweka rekodi ya kufunga bao la kwanza msimu wa 2020/21.

Alipachika bao dakika ya 68 kwenye Uwanja wa Majaliwa mjini Ruangwa, na kumfanya mchezaji huyo raia wa Burundi kuweka rekodi hiyo, akiisaidia pia timu yake ya Namungo kupata ushindi wa bao 1-0. Ni kwa sababu ndiyo mechi iliyochezwa mapema zaidi na tano zilizofuata zilichezwa baadaye.

**#2. Lambart Subianka (Prisons)**

Ni straika wa Prisons ambaye aliweka rekodi ya kufunga bao la mapema zaidi kwenye mechi za raundi ya kwanza ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Bao lake la dakika ya saba dhidi ya Yanga na kuifanya timu yake kutoka sare ya 1-1, lilimfanya kuwa mfungaji wa bao la mapema zaidi kwenye mechi za raundi ya kwanza ya Ligi Kuu Bara.

**#3. Omari Mponda (Ihefu FC)**

Omari Mponda ambaye ni straika wa Ihefu, yeye ameweka rekodi ya kufunga bao dhidi ya Simba kwa mara nyingine tena kwenye mechi ya ufunguzi. Alifunga la kufutia machozi Jumapili iliyopita kwenye mechi ambayo timu yake ilifungwa mabao 2-1.



John Bocco

Mponda alishawahi kufanya hivyo kwenye Ligi Kuu msimu wa 2016/17 katika Uwanja wa Benjamin Mkapa wakati akiichezea Ndanda FC.

Kwenye mechi ya ufunguzi ambayo Simba ilishinda mabao 3-1 Agosti 20, 2016, straika huyo alifunga bao la kufutia machozi.

**#4. John Bocco (Simba SC)**

Straika John Bocco wa Simba, amevunja rekodi ya mabao ya ufunguzi wa Ligi Kuu ya timu hiyo kufungwa na wachezaji wa kigeni kwa misimu mitano mfululizo.

Bao la dakika ya 11 kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya dhidi ya Ihefu, lilimfanya mchezaji huyo kuwa mchezaji wa kwanza kuifungia timu yake bao msimu huu na kumaliza ubabe wa wachezaji kutoka nje ya nchi ambao kwa misimu mitano ndiyo waliokuwa wakiibeba Simba kwa kufunga mabao ya kwanza ya msimu.

Mara ya mwisho bao la kwanza la msimu kwa Simba kufungwa na mzawa ilikuwa Septemba 21, 2014, msimu wa 2014/15, wakati Shaaban Kisiga alipofanya hivyo kwenye mechi ya ufunguzi kati ya Simba na Coastal Union na timu hizo kutoka sare ya mabao 2-2.

Baada ya hapo Mganda Hamisi Kiiza, Emmanuel Okwi, Mrundi Laudit Mavugo, na Mnyarwanda Meddie Kagere ambaye alifunga mabao ya kwanza kwenye klabu hiyo kwa misimu miwili mfululizo, ndio wamekuwa wakitamba.

**#5. Prince Dube (Azam FC)**

Straika mpya wa Azam FC kutoka nchini Zimbabwe, Prince Dube amekuwa mchezaji wa kwanza kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara kufunga mabao mawili kwenye mechi moja. Alifanya hivyo Septemba 11 kwenye mechi ya raundi ya pili ya Ligi Kuu ambayo timu yake ilicheza dhidi ya Coastal Union.

Alipachika bao la kwanza kwake yeye tangu ajiunge na Azam na pia kwa timu yake kwenye mechi hiyo, dakika ya 68, huku la pili akilifunga kwenye dakika ya 88 na kumfanya kuweka rekodi hiyo msimu huu.

Amefanya kama alivyofanya straika wa Simba, Meddie Kagere ambaye msimu uliopita ndiye aliyekuwa mchezaji aliyeweka rekodi hiyo, akifunga mabao mawili kwenye mechi dhidi ya JKT Tanzania, ikiwa ni mchezo wa ufunguzi wa Ligi Kuu, dakika ya kwanza na 58.

**JE, WAJUA?**



WILLIAN amekuwa mchezaji wa kwanza Arsenal, kuweza kutoa pasi mbili za mwisho/mabao ['assists'] kwenye mechi ya Ligi Kuu England akiichezea klabu hiyo, kwa mara ya kwanza tangu Ray Parlour alipofanya hivyo mwaka 1992. Willian alifanya hivyo juzi wakati wakishinda 3-0 ugenini kwenye mechi ya kufungua msimu dhidi ya Fulham.





# Vyama vya siasa vyatakiwa kuwapa fursa wenye ulemavu

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

VYAMA vya siasa nchini, vimeombwa kuendelea kuwapitisha watu wenye ulemavu kugombea nafasi mbalimbali kwenye uchaguzi kwa kuwa wana uwezo wa kuongoza.

Katibu wa Shirikisho la Vyama vya Watu wenye Ulemavu (SHIVYAWATA), Mkoa wa Dodoma, Justust Ng'wantalima, alitoa rai hiyo wakati akitoa wasilisho la mrejesho wa mkutano wa utambulisho wa mradi na mafunzo juu ya haki ya watu wenye ulemavu kushiriki kwenye michakato ya uchaguzi mkuu wa 2020.

Alipongeza kuwa katika uchaguzi wa mwaka huu, vyama vimetambua uwezo wa watu wenye ulemavu na kuwapitisha kugombea nafasi mbalimbali za ubunge na udiwani, tofauti na uchaguzi uliopita.

"Kwa kweli shirikisho tuna kila sababu ya kuvipongeza vyama vya siasa kwa kuwadhamini makundi haya maalum na kuwateua kuwa wawakilishi wao ili kugombea nafasi za ubunge na udiwani, hii inaonyesha ni jinsi gani tunavyotambuliwa kutokana na uwezo walionao," alisema.

Aidha, katibu huyo alisema shirikisho hilo litaendelea kuelimisha jamii juu ya uwezo walionao wa watu wenye ulemavu ili waendelee kuaminiwa zaidi.

Alieleza kuwa watu hao wamejengewa uwezo wa kuzitambua fursa zilizopo na wachangamkia ili kutonyanyapaliwa.

"Kutokana na dhana potofu iliyojengeka kwa baadhi ya jamii ya unyanyapaa kwa watu wenye ulemavu, shirikisho hili litaendelea kutoa elimu ili walemavu waaminiwe na kupatiwa nafasi zaidi za maamuzi ndani ya vyama vya siasa na serikalini," alisema.

Aliomba vyama vya siasa kuendelea kutoa nafasi mbalimbali za uongozi kwa watu wenye ulemavu wenye sifa na vigezo ili kubadili mtazamo hasi wa jamii dhidi yao.

Naye mmoja wa washiriki katika mkutano huo, Dekariswa Mmari, aliwataka wagombea ambao hawakuchaguliwa kwenye michakato ya uchaguzi ndani ya vyama kuwa watulivu na watoe mawazo kwa waliopitishwa ili kuleta maendeleo kwa Watanzania.

Aliwaasa wagombea kunadi sera zenye mashiko kwa Watanzania na watu wenye ulemavu kwenye majukwaa ya kampeni ili kuwaweka Watanzania pamoja.




Katibu wa Shirikisho la Watu wenye Ulemavu Mkoa wa Dodoma (SHIVYAWATA), Justust Ng'wantalima (kulia), akitoa wasilisho la mrejesho wa mkutano wa utambulisho wa mradi na mafunzo juu ya haki ya watu wenye ulemavu kushiriki kwenye michakato ya uchaguzi mkuu wa 2020 kwa washiriki wa vyama vya watu wenye ulemavu iliyofanyika mjini Dodom jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Taasisi zaombwa kushirikisha wanawake

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imezitaka taasisi na mashirika ya umma kuwashirikisha wanawake kwenye mipango yao.

Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Dk. Francis Michael, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipokuwa akifungua kikao kazi cha kujadili rasimu ya mwongozo wa ujumuishaji masuala ya jinsia katika utumishi wa umma, jijini hapa.

Dk. Michael alisema serikali imeandaa rasimu hiyo ambayo itatoa maelekezo ya namna ya kujumuisha masuala ya kijinsia mahala pa kazi na kujenga mazingira bora na wezeshi kwa makundi mbalimbali kwenye taasisi za umma.

Alisisitiza waajiri kuwa, pendekezo la urithishanaji madaraka kuzingatia suala la kijinsia lipewe umuhimu mkubwa kwa kuhakikisha wanawake wanapata fursa kujumuishwa kwenye mipango ya mafunzo ili kujengewa uwezo kiutendaji.

"Uzoefu umekuwa ukionyesha kina mama wanalalamika lakini malalamiko yao hayatiliwi mkazo, lalamiko likija mezani kwako, lazima ulifanyie kazi vyema tena haraka," alisema.

Aliwahimiza umuhimu wa rasimu hiyo kuyawezesha makundi yote kutekeleza wajibu wao kwa ufanisi katika utumishi wa umma.

Aliwataka viongozi katika utumishi wa umma kuhakikisha wanabaini watumishi wenye vipaji maalum kutoka makundi anuai na kuviendeleza vipaji hivyo.

"Pia muangalie namna ya kuanzisha vituo vya malezi kwa watoto katika majengo ya ofisi za umma, ili mtumishi anayenyonyesha atumie muda wake kikamilifu katika kutekeleza majukumu ya kikazi," alisema.

Naye Mkurugenzi Msaidizi Anuai za Jamii wa Ofisi hiyo, Leila Mavika, alisema tofauti na mwongozo wa mwaka 2010, rasimu hiyo inayoboreshwa imezingatia masuala ya jinsia na usimamizi wa rasilimali watu.

"Hivyo mwongozo huu ukiidhinishwa rasmi kutumika utakuwa ni mahsusi kuratibu ujumuishwaji wa masuala ya jinsia katika usimamizi wa rasilimali watu kwenye utumishi wa umma, kwa kuwa uzingatiaji wa masuala ya kijinsia unaongeza tija, pato la taifa na huduma za kijamii," alisema.

# Wamachinga kutengewa eneo kubwa Dodoma

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma, imejipanga kujenga eneo maalum Nzuguni kwa ajili ya wafanyabiashara wadogo ambalo ni kubwa zaidi ya Kariakoo.

Akizungumza jana na Nipashe, Mkurugenzi wa Jiji hilo, Joseph Mafuru, alisema eneo hilo lina ukubwa wa hekta 13.4 na litajengwa mwaka wa fedha 2020/21.

"Pale Nzuguni tutajenga eneo la 'Pet traders' hawa wafanyabiashara wadogo, yaani sio kama Kariakoo, yaani lenyewe ni sawa na kuunganisha Kariakoo na Ubungo pamoja. Soko la Ndugai chukulia ndio Kariakoo halafu stendi ya Nzuguni chukulia ni Ubungo sasa sisi tumeweka pamoja," alisema.

Alisema eneo hilo litakuwa katikati ya stendi na soko hilo na Jiji litawapatia maeneo kwa gharama rahisi ili kupanga bidhaa zao.

"Yaani kutakuwa na amsha amsha ya kutosha, wafanyabiashara wakifika kule watakuta tumewaandalia maeneo ya kutosha kwa ajili yao na pale stendi ya daladala tumeandaa ramani ya kujenga vizimba, lakini masoko yenyewe bado hayajajaa," alisema.

Alisema mbele ya Soko la Ndugai kuna vizimba 400 vitajengwa katika mwaka huu wa fedha 2020/21, ili kukidhi mahitaji ya wafanyabiashara wadogo.

Alisema masoko yaliyopo jijini humo yanatosha kubeba wafanyabiashara hao.

"Kwa mfano soko la Ndugai wafanyabiashara taratibu wanaanza kusogea kule, kilichochelewesha ilikuwa ni tatizo la usafiri ambalo limeshughulikiwa sasa," alisema.

Mafuru alisema wakati soko hilo linaanza lilisuasua kutokana na tatizo hilo, lakini kwa sasa yametolewa mabasi yaliyokuwa eneo la Nanenane na kupelekwa sokoni hapo hali iliyochangia sasa wafanyabiashara kufanya biashara zao.

"Pale ukienda sasa kuna amsha amsha za kufa mtu, idadi ya wafanyabiashara na wateja imeanza kuongezeka katika soko hilo, kuna watu wanafikiri huu mji hapa ndio katikati ya mji ukweli ni kwamba huu utakuja kuwa mji wa kale, Centre (kitovu) cha mji ni Nzuguni, shughuli nyingi zitafanyika kule," alisema.

Alisema suala la wafanyabiashara kufanya biashara kando kando ya barabara katikati ya mji lipo mbioni kuondoka kutokana na maeneo yaliyoandaliwa kwa ajili yao.





## CCM yaahidi kupaisha maendeleo Mbeya Mjini

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MBUNGE mteuli wa Viti Maalum Mkoa wa Mbeya, Maryprisca Mahundi, amedai kuwa endapo wakazi wa Jimbo la Mbeya Mjini watakipa ridhaa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuongoza jimbo hilo, watahakikisha wanatatua kero zote zinazowakabili zikiwamo za sekta ya elimu, afya, maji, kilimo na miundombinu.

Mahundi aliyasema hayo juzi wakati wa kampeni za kumnadi mgombea wa chama hicho, Dk. Tulia Ackson kwenye maeneo ya kata mbalimbali za Jiji la Mbeya.

Alisema wananchi wakiipa kura za kutosha CCM watafurahia maisha kwa sababu wataboreshewa huduma mbalimbali za kijamii kuliko wakikipa chama kingine watapata majuto.

"Katika kampeni zetu tumewaeleza wananchi kuwa endapo wakitupa nafasi tutatua matatizo yao, lakini tumewahimiza kumpigia kura za mfano Rais John Magufuli kwa sababu ya mambo makubwa aliyotufanyia, hakuna ambaye hayaona uboreshaji katika sekta ya elimu, maji, afya, mikopo, miundombinu ya barabara, meli, reli na anga," alisema Mahundi.

Aliongeza kuwa kipindi cha miaka 10 ambacho jimbo hilo lilikuwa mikononi mwa upinzani hakuna maendeleo yaliyofanyika kwa manufaa ya wananchi zaidi ya mbunge aliyekuwapo kujinufaisha binafsi.

Aidha, mbunge huyo aliwaomba kina mama kukupigia kura CCM kwa madai kuwa kimebeba ajenda ambazo zimelenga kumsaidia kujikwamua kiuchumi kupitia mikopo, vipaumbele vya ajira na fursa za kibiashara.

Mgombea udiwani kwa tiketi ya CCM, Majengo, Maulid Issa, alisema moja ya vipaumbele vyake ni kuboresha mazingira ya utoaji mikopo ya asilimia 10 inayotolewa na halmashauri kwa ajili ya kuviwezesha vikundi vya wanawake, vijana na wenye ulemavu, kulegeza masharti ambayo miongoni ni kuhimiza wahitaji lazima wawe na shughuli za kufanya kwanza ndipo wapate mikopo.

Aliongeza kuwa kazi kubwa atahamasisha wanawake kujiunga na vikundi mbalimbali vya ujasiriamali na kwamba atakuwa anatoa kiasi cha fedha ili kuongeza uzalishaji.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Mbeya, Mchungaji Jacob Mwakasole, aliwaomba wananchi kufanya uchaguzi sahihi wa wagombea kwa kuhakikisha wanamchagua mtu makini ambaye ataweza kubeba ajenda zao na kuzisemea kwenye vyombo vya maamuzi.

# Mazao ya bustani kunufaisha maelfu ya wakulima wadogo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKULIMA wadogo wa mazao ya bustani 75,000 wanatarajiwa kupatiwa elimu ya kilimo bora cha mboga, matunda na viungo katika mikoa ya Mbeya, Songwe na Katavi ili kuongeza uzalishaji utakaosaidia kwenye ukuaji wa uchumi jumuishi na kuongeza usalama wa chakula.

Elimu hiyo inatarajiwa kutolewa na Shirika lisilokuwa la kiserikali liitwalo HELVETAS Tanzania kupitia mradi wa kilimo bora cha mboga na matunda kwa wanawake na vijana (KIBOWAVI) chini ya ufadhili wa Umoja wa Ulaya (EU).

Mkurugenzi wa HELVETAS Tanzania, Daniel Kalimbiya, aliyasema hayo juzi wakati wa kufunga mafunzo ya mbinu bora za kilimo cha mazao ya bustani kwa watoa huduma binafsi (LSPs) yaliyotolewa kwa ushirikiano kati ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI) Kituo cha Uyole na Chuo cha Mafunzo ya Mboga, Matunda na Maua cha Tengeru.

Alisema wanufaika wa mafunzo hayo watatoka katika kaya 15,000 kutoka kwenye halmashauri zote za mikoa hiyo mitatu, na kwamba pia vikundi 500 vya wakulima na taasisi za wasindikaji vitanufaika na elimu hiyo.

"Mradi huu ni wa miaka mitano na tunautekeleza kwa ushirikiano na taasisi zingine kama CODERT, ADP Mbozi, na TAFOPA, gharama ya mradi ni Euro 5,000,000 ambazo asilimia 95 tunafadhiliwa na EU na asilimia inayobaki ni michango ya washirika," alisema Kalimbiya.

Vilevile, alisema vitaanzishwa vituo vya mafunzo kwenye kila halmashauri ambavyo wananchi watakuwa wanaenda kupata mafunzo mara kwa mara ya uzalishaji wa mazao ya bustani.

Mkurugenzi wa Chuo cha Mafunzo ya Mboga, Matunda na Maua cha Tengeru kilichopo mkoani Arusha, Juma Shekidele, alisema mikoa ya Kanda ya Kaskazini ina uzoefu mkubwa kwenye uzalishaji wa mazao ya bustani.

Alisema mazao hayo yana faida kubwa kiuchumi na hivyo akawataka wananchi wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kuchangamkia fursa ya kuyazalisha kwa maelezo kuwa mikoa hiyo ina hali nzuri ya hewa inayoruhusu kustawi.

Alisema mikoa ya Kanda ya Kaskazini ina uzoefu wa zaidi ya miaka 40 kwenye uzalishaji wa mazao hayo na kwamba asilimia kubwa ya mazao hayo yanasafirishwa nje ya nchi.

"Huku kuna hali nzuri ya hewa ambayo inaruhusu kustawi mazao hayo, tena kuna miundombinu mizuri ya usafirishaji ukiwamo uwanja wa ndege wa Songwe na reli ya Tazara," alisema Shekidele.

Ofisa Kilimo Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Merius Nzalawahe, alilipongeza HELVETAS kwa kuanzisha mradi huo kwa maelezo kuwa kilimo cha mazao ya bustani ni miongoni mwa mazao yanayoliingizia taifa fedha nyingi.

Alisema mazao hayo ya bustani yamepata umaarufu hivi karibuni kwa maelezo kuwa miaka ya nyuma baada ya uhuru, serikali ilitilia mkazo kwenye kilimo cha mazao ya biashara kutokana na kwamba yalikuwa yanaliingizia taifa fedha nyingi.

Alisema kwa sasa mazao ya bustani yanaliingizia taifa fedha nyingi za kigeni kuliko hata mazao ya biashara na kwamba ndiyo maana serikali imeanza kuhamasisha wananchi kuyazalisha kwa kushirikiana na sekta binafsi.



Naibu Waziri wa Kilimo, Omary Mgumba (mwenye shati jeupe), akiwaonyesha kitu viongozi wa Wilaya ya Mbarali, mkoani Mbeya juzi, alipofanya ziara ya kukagua miradi ya kilimo vikiwamo viwanda vya kukoboa mpunga na skimu za umwagiliaji. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Fedha kutozwa kutunisha mfuko wa umwagiliaji

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

SERIKALI imesema inakusudia kuanza kuwatoza fedha wakulima wanaotumia skimu za umwagiliaji, ili kutunisha mfuko wa umwagiliaji nchini utakaosaidia kwenye ujenzi wa miundombinu mipya na kuboresha iliyopo.

Naibu Waziri wa Kilimo, Omary Mgumba, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati alipokuwa anazungumza na wakulima na wamiliki wa viwanda vya kukoboa mpunga wilayani Mbarali ikiwa ni mwendelezo wa ziara yake ya kukagua miradi ya kilimo na kusikiliza kero za wakulima.

Alisema kwa muda mrefu ujenzi wa skimu za umwagiliaji na uboreshaji iliachiwa serikali peke yake jambo ambalo ni kinyume na Sera ya Umwagiliaji ya Mwaka 2013 ambayo ilielekeza kuanzishwa kwa mfuko wa umwagiliaji.

Alisema wakulima wanaotumia skimu hizo watakuwa wanachangia kama ilivyo kwenye vituo vya afya na zahanati za serikali ambazo wananchi wanachangia kwenye ujenzi na upanuzi na sio kuiachia serikali pekee itekeleze jukumu hilo.

"Sera yetu ya umwagiliaji inatutaka tuanzishe mfuko wa umwagiliaji, lengo kuu ni serikali kukusanya fedha ili tuwapanulie skimu zilizopo zichukuwe eneo kubwa zaidi na tuanzishe nyingine ambazo zitawasaidia kuboresha kilimo," alisema Mgumba.

Alisema Wilaya ya Mbarali ni miongoni mwa maeneo nchini yenye skimu nyingi za umwagiliaji na kwamba serikali huwa inatumia fedha nyingi kuboresha miundombinu ya skimu hizo.

Awali Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, alimweleza Naibu Waziri huyo kuwa kuna tatizo la wanachama wa skimu za umwagiliaji wilayani humo kutojitolea kuchangia uboreshaji wa miundombinu licha ya kuwa wanapata manufaa makubwa.

Alisema tatizo hilo wakati mwingine huwa linasababisha wakulima kuchelewa msimu wa kilimo kwa sababu ya kuisubiria serikali ifanyie matengenezo ya miundombinu ambayo inakuwa imeharibika.

"Asilimia kubwa ya mpunga unaozalishwa katika wilaya hii unatokana na umwagiliaji, tuna skimu nyingi sana za umwagiliaji ambazo ndio chanzo kikuu cha uzalishaji wetu huu, wakulima wananufaika sana lakini tatizo hawako tayari kuchangia kwa hiari uboreshaji wa miundombinu," alisema Mfune.

Hata hivyo, baadhi ya wananchi walipinga hatua hiyo ya serikali kutaka kuanza kuwatoza fedha hizo za kuchangia miundombinu kwa madai kuwa wao wanatoa ushuru wa meza.

Mmoja wa wananchi hao, Theresia Mwakangale, ambaye ni mkazi wa Mji wa Ubaruku na mkulima wa mpunga wilayani humo, alisema uboreshaji wa miundombinu ni jukumu la serikali na sio la wakulima ambao wanatoa ushuru.

Alisema wakati mwingine huwa wanatumia gharama kubwa kusafirisha mazao yao kutoka mashambani kwenda kwenye maghala na sokoni kutokana na ubovu wa miundombinu na hivyo serikali kuanza kuwatoza fedha za kuboresha skimu ni kuwaongezea gharama.

Naibu Waziri Mgumba anaendelea na ziara ya kikazi mkoani Mbeya, ambapo moja kati ya shughuli anazozifanya ni kuwatembelea wakulima, kutembelea vituo na taasisi za utafiti kwa lengo la kuhamasisha kilimo.



# MCT yataka weledi uandishi wa habari za uchaguzi mkuu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KATIBU wa Baraza la Habari Tanzania (MCT) Kajubi Mukajanga, amewataka waandishi wa habari kujitahidi kutoa habari bila ya upendeleo katika kipindi hiki cha kampeni kuelekea uchaguzi mkuu.

Aliyasema hayo Visiwani Zanzibar alipotembelea vyombo vya habari Zanzibar akiongozana na bodi ya maadili ya baraza hilo.

Alisema ni wajibu wa waandishi wa habari kutenda haki na kutoegemea upande mmoja wakati wa kuandika habari za kampeni.

Alisema watakapotenda haki kwa vyama vyote, viongozi wa vyama vya siasa watakuwa na imani na waandishi wa habari.

Aidha, aliwataka waandishi wa habari kuzingatia maadili ya taaluma hiyo ili kuepukana na matatizo ambayo yaweza kujitokeza.

Aliwataka waandishi wa habari na watangazaji kuepuka kutumia lugha zisizofaa.

Naye mjumbe wa bodi ya maadili ya baraza hilo, Eda Sanga, aliwataka waandishi wa habari kuacha kufanya kazi kwa mazoea na badala yake kufika kwa jamii kuibua changamoto zinazowakabili.

Aliwataka watangazaji na waandaaji wa vipindi vya redio na runinga kuwa wabunifu na kuibua vitu vipya ili kupata wasikilizaji wengi.

"Kazi ya redio au televisheni ni kama kazi ya mgahawa wa chakula, kila siku wateja wanataka chakula kipya na kizuri," alisema.

Alisema ni vyema kuandaa vipindi vyenye kuakisi matakwa na mahitaji ya jamii.



Katibu wa Mufti, Khalid Ali Mfaume, akimkabidhi misahafu Mkuu wa Wilaya Magharibi 'A' katika uzinduzi wa ugawaji kwa wilaya zote za Zanzibar mwishoni mwa wiki. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# DC atoa angalizo ajali za barabarani

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKUU wa Wilaya ya Kaskazini 'B', Unguja Rajab Ali Rajab, amewataka watumiaji wa vyombo vya moto hasa pikipiki kuzingatia sheria za usalama barabarani katika kipindi chote cha mikutano ya kampeni.

Amesema tahadhari hiyo lengo lake ni kuepusha ajali ambazo zimekuwa zikisababisha kupotea kwa nguvu kazi ya taifa pamoja na ulemavu wa kudumu.

Aliyasema hayo wakati akizungumza na baadhi ya vijana wakati wa uzinduzi wa maandamano ya waendesha pikipiki na bodaboda kupitia Jumuiya ya Vijana ya Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) Wilaya ya kaskazini 'B' zilizoanzia katika ofisi za CCM Mahonda.

Alisema katika kipindi cha kampeni ajali nyingi zimekuwa zikitokea kutokana na watumiaji wa vyombo hivyo kushindwa kutii sheria za usalama barabarani.

Alieleza kuwa vijana ndio nguvu kazi ya taifa, hivyo ni vyema kutokubali kutumiwa na baadhi ya wanasiasa kufanya vurugu na badala yake watumie nafasi zao kwa kuhubiri amani ili viongozi watakaochaguliwa walete maendeleo.

Aliwataka vijana kuacha kujihusisha na uuzaji na usamabazaji wa dawa za kulevya badala yake washirikiane na vyombo vya ulinzi na usalama kuwafichua wafanyabiashara hiyo ili waweze kuchukuliwa hatua za kisheria

Naye Mkuu wa Usalama Barabarani Wilaya ya Kaskazini 'B', Meja Pandu Jecha Pandu, alisema Jeshi la Polisi ndani ya wilaya hiyo limejipanga vyema kwa wote ambao watakaokiuka taratibu na sheria zilizowekwa na jeshi hilo ikiwamo uvaaji wa kofia ngumu na kutokuwa na leseni.

Kwa upande wao baadhi ya waendesha pikipiki na bodaboda wameuhakikishia uongozi wa wilaya kuwa watashirikiana katika kipindi chote cha kuelekea uchaguzi mkuu kwa kuhakikisha amani na utulivu vinaendelea kuwapo.

Zaidi ya vijana 60 walishiriki uzinduzi huo ambao ulikuwa na lengo la kuhamasisha vijana kutii sheria za usalama barabarani katika uchaguzi mkuu pamoja na kulinda amani nchini.

## Katibu wa Mufti awapa ushauri viongozi wa dini

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIBU wa Mufti wa Zanzibar, Sheikh Khalid Ali Mfaume, amewashauri Maimamu na Makhatibu wa Misikiti pamoja na walimu wa madrasa wa Qur ani kuhubiri amani wakati nchi inaelekea kwenye uchaguzi mkuu.

Sheikh Khalid alitoa ushauri huo kwenye uzinduzi wa ugawaji mashafu kwenye madrasa za Qur-an za wilaya zote za Zanzibar yaliyotolewa na Jumuiya ya Maendeleo ya Kiislamu ya Al Salaam ikishirikiana na Ofisi ya Mufiti Zanzibar. Hafla hiyo ilifanyika katika Ofisi ya Halmashauri ya Wilaya Magharibi 'A' Kianga Unguja.

Alisema wananchi wanahitaji amani, hivyo mahubiri yatakayotolewa na Mashekhe na Maimamu wa misikiti yaelekezwe katika kuimarisha umoja, amani na utulivu.

Alikumbusha kuwa dini ya Kiislamu haishawishi fujo bali inahimiza amani na ushirikiano, hivyo aliwataka viongozi hao kuelekeza mahubiri yao kama dini inavyoelekeza.

"Usalama na amani ndio mtaji wetu, bila ya amani hakuna maisha nani ataweza kutoka kutafuta mahitaji ya familia yake wakati nchi inafujo?" Alihoji Katibu wa Mufti.

Aliwaeleza walimu wa madrasa za Qur an kuacha tabia ya kuwaingiza wanafunzi wao kwenye misimamo ya kisiasa na kufanya hivyo ni kuwapeleka katika matatizo bila ya muda wao kufika.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Magharibi "A", Abeid Juma Ali, ambaye alikuwa mgeni rasmi katika uzinduzi huo, aliwanasihi viongozi wa dini kuendelee kutoa mahubiri yanayoelekezea jamii katika ustawi mzuri wa maisha yao.

Alisema kuwa wilaya yake haitamvumilia kiongozi yeyote wa dini atakayeanzisha mahubiri ya kushawishi waumini wao kuvunja sheria za nchi.

Abeid aliishukuru Serikali ya Kuwait kwa misaada mbalimbali inayotoa kwa Jumuiya ya Kiislamu ya Al Salaam, ambayo imeanza kuwasaidia wananchi wa Zanzibar.

Akizungumzia lengo la kuanzishwa kwa Jumuiya ya Al Salaam katika hafla hiyo Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo, Sheikh Khamis Masoud, alisema wamekusudia kujenga Chuo Kikuu cha Kiislamu na Jengo la Dakhalia kwa ajili ya wanafunzi wa kike.

Jumuiya hiyo imeanza kusambaza zaidi ya mas-hafu 336, 000 iliyotolewa msaada na Serikali ya Kuwait kwa ajili ya vyuo vya wilaya zote za Zanzibar na wameanza na Wilaya ya Magharibi 'A'.

## MATANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### VIWANJA/MASHAMBA

**KIWANJA KINAUZWA,** Kiwanja cha Biashara kinauzwa Regent Estate Dsm mita za mraba 1300. Piga; 0693 689996, 0757 129546.


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

**Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676**


---

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**

**DISTRICT AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION**

**CAUSE NO.....6.....OF 2020**

In the matter of the Estate of the late...**ELIZABETH CANDIOS HYERA**
**BY 1...STELLA ALEX HUMBI**
**2.................**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceeding if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above- named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 29 day of September...2020

Dated at MOROGORO this.. 07...day of September ...2020

RESIDENT MAGISTRATE

115899202

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**(MCA/84)**

**Katika mahakama ya mwanzo ya MJINI Wilaya ya KILOSA**

**MADAI NAMBARI 42 YA 2020**

**MDAI DORISI KISANGA**

**MDAIWA DANIEL MALISA**

**MADAI FEDHA SHS 6,500,000/=**

**KWA: DANIEL MALISA**
**POPOTE ULIPO**

Unaamrishwa na JAMHURI uhudhurie mbele ya Mahakama hii siku ya JUMATATU,Tarehe 21/09/2020 saa 2:30 Asubuhi/Alasiri kuwa ni mdaiwa katika shauri lililotajwa hapo juu na ukifika usiondoke bila ya ruhusa ya Mahakama na unaonywa kwamba ikiwa utapuuza wito huu bila ya udhuru wa maana hati itatolewa kukulazimisha kuhudhuria.

Hati hii inatolewa kwa amri yangu na muhuri wa mahakama hii leo 19/08/2020.
Kuitwa shaurini hii imetolewa kwa maombi ya:
DORIS KISANGA
KILOSA.

HAKIMU

115899102

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**Katika Mahakama ya mwanzo MAKOLE wilaya ya DODOMA - MJINI**

**MADAI NAMBARI 12/2020**

**MDAI ................................ CONSTANSIA NELSON**

**DHIDI YA**

**MDAIWA ..................................GODWIN ZAKARIA**

**KWA: GODWIN ZAKARIA**
**Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba**
**Madai ya TALAKA**

Hivyo unahitajiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii siku ya Jumatatu Tarehe 16/09/2020 saa 2.30 asubuhi kwa kujibu madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ya kukatwa shauri hilo ni lazima kuleta mashidi wako na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.
Angalia kama *hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu Mahakama ikidhibitisha kama *umepokea kuitwa shaurini hii, itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na Chapa ya Mahakama hii leo tarehe 09/09/2020.

115899002

---

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**LOOKEN FRAELI SWAI** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA **TOYOTA HIACE** YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 335 AYV.** YENYE CHASSIS NAMBA **LH71V0009678.** YEYOTE ATAKAYE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. **Control No: 9910818971257.**

115898802


**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Waokoaji DR Congo wachimba vifusi mgodini

KINSHASA, DRC

WAOKOAJI wamechimba vifusi kufuatia kuporomoka kwa mgodi wa dhahabu nchini DR Congo na kusababisha watu takriban 50 kufariki dunia.

Mgodi huo uliopo karibu na mji wa Kamituga, mashariki mwa taifa hilo uliporomoka siku ya Ijumaa kufuatia mvua kubwa.

Maofisa wa eneo hilo wanasema kwamba wengi wa wale wanaohofiwa kufariki ni vijana wadogo na sasa wametoa wito wa siku mbili za maombolezi.

Ajali ni vitu vya kawaida katika sekta ta migodi nchini DR Congo ambayo ina viwango duni vya usalama.

Mauzo ya dhahabu yapanda Uganda na kuzua mjadala.

Kanda za video zilionyesha watu wakijaribu kuchimba vifusi hivyo vilivyokuwa vinaziba mlango wa mgodi huo, huku waokoaji wakitumia vifaa wengine mikono yao kuondoa vifusi hivyo.

Gavana wa eneo hilo la mkoa wa kusini mwa Kivu, Theo Kasi, alisema kwamba ameshtushwa na vifo hivyo vya watu 50 wengi wao wakiwa vijana.

Hata hivyo, Meya wa mji wa Kamituga, Alexandre Bundya, alisema, hatuna hakika kuhusu idadi ya waliofariki, kilisema chombo cha habari cha AFP.

Shahidi mmoja aliiambia AFP kwamba mvua kubwa ilisababisha maji kuingia katika mgodi huo, wakati watu walipojaribu kutoka, kulikuwa hakuna njia kwasababu maji yalikuwa yanaingia kwa wingi.

Mikasa ya kuporomoka kwa migodi hutokea mara nyingi katika nchi mbalimbali duniani, na watu wamekuwa wakipoteza maisha kutokana na hali hiyo.

Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo ni nchi tajiri kwa dhahabu, almasi na coltan lakini migodi mingi inadhibitiwa na makundi yenye silaha.

Watu wa DRC ni miongoni mwa watu maskini zaidi barani Afrika ingawa nchi hiyo ni tajiri kwa rasilimali.



Uokoaji wa watu wanaodaiwa kufukiwa na kifusi katika mgodi wa dhahabu karibu na mji wa Kamituga Mashariki mwa DRC ukiendelea. **PICHA: BBC**

# Mgogoro wa Libya wajadiliwa kimataifa

CAIRO, Misri

SUALA la Libya linajadiliwa kwa wiki kadhaa katika miji mikuu kadhaa ya kimataifa kwa lengo la suluhisho kwa mgogoro unaoendelea nchini humo tangu kuuawa kwa aliyekuwa kiongozi wa nchi hiyo Muhammad Gaddafi.

Baada ya majadiliano wiki hii huko Bouznika nchini Morocco na huko Geneva kati ya maofisa wa Libya kutoka kambi mbili hasimu, hatimaye mikutano inafanyika katika mji mkuu wa Misri, Cairo, na ujumbe wa viongozi 10 kutoka Magharibi mwa Libya wanaounga mkono serikali ya umoja wa kitaifa (GNA) inayotambuliwa na jamii ya kimataifa.

Kulingana na vyanzo vyetu, mazungumzo ambayo yatafanyika hadi Jumapili, Septemba 13 yanafanyika katika "mazingira mazuri" na yanalenga kurudisha uhusiano na Misri, mshirika mkubwa wa Marshal Khalifa Haftar, mbabe wa kivita Mashariki mwa Libya.

"Ushirikiano huu na Misri sasa unafanyika kwa sababu mambo kwa sasa yamebadilika," Saad Benshrada, mmoja wa wajumbe na Ofisa wa Baraza Kuu la Serikali nchini Libya amemwambia Houda Ibrahim, wa wa kitengo cha RFI katika ukanda wa Afrika (RFI Afrique).

"Walibya pamoja na jamii ya kimataifa wanaona kuwa hakuna upande katika mapambano unaoweza kushinda mwingine kwa kwa kutumia silaha. Mazungumzo pekee ndio yamesalia kama njia ya kuiokoa Libya," ameongeza.

Saad Benshrada amesema ana matumaini kwamba "Misri, kwa kuwa ina uhusiano na Marshal Khalifa Haftar na Aguila Saleh [Spika wa bunge la Libya] inaweza kuwashawishi wawili hao ili kufikia mkataba wa kudumu wa kusitisha vita, kuanza tena uzalishaji wa mafuta na kukubali matokeo ya majadiliano yoyote kati ya Walibya katika siku zijazo".

"Tunajua kwamba Misri ni nchi muhimu kwa Libya na kwamba hakutakuwa na suluhisho kwa nchi yetu bila kuishirikisha Cairo," Saad Benshrada amebaini. Tumewaambia lawama zetu lakini zilikuwa shutuma kati ya ndugu. Majadiliano yetu ni mazuri. Sisi sote tunataka kufunua ukurasa mpya na kufikiria juu ya siku zijazo.

Tumeitaka Misri kudumisha mawasiliano na Magharibi mwa Libya na WaLibya wote kote nchini. Tunajua vizuri kwamba Misri ni mshirika mkubwa, hodari na mwenye nguvu katika Mashariki ya Kati.

*RFI*

## Ilan yaicharukia Bahrain tuhuma usaliti wa Israel

TEHRAN, Iran

IRAN imeinyooshea kidole cha lawama Bahrain kwa kile ilichoita msaidizi wa uhalifu wa Israeli, siku moja baada ya kutangazwa kwa makubaliano ya kurejesha uhusiano kati ya nchi hizo mbili.

"Viongozi wa Bahrain sasa watahusishwa katika uhalifu wa utawala wa Kizayuni, kama tishio la mara kwa mara kwa usalama wa ukanda mzima wa Mashariki ya Kati na ulimwengu wa Kiislamu," Wizara ya Mambo ya Nje ya Iran imesema katika taarifa.

Israeli na Bahrain zilifikia makubaliano ya kufufua uhusiano wao Ijumaa (Septemba 11), mwezi mmoja baada ya makubaliano kati ya Falme za Kiarabu na nchi hiyo ya Kiyahudi.

Katika taarifa ya pamoja, Marekani, Bahrain na Israeli zimesema kuwa kufungua mawasiliano ya moja kwa moja na ushirikiano kati ya pande hizo mbili na chumi zilizoimarika kutaendelea kuleta mabadiliko ya manufaa katika eneo la Mashariki ya Kati na kuongeza uthabiti, usalama na ufanisi katika eneo hilo.

Ikulu ya White House nchini Marekani imesema Rais Donald Trump alitoa tangazo hilo kupitia ukurasa wake wa twitter baada ya kuzungumza kwa njia ya simu na mfalme wa Bahrain Hamad bin Isa Al Khalifa na waziri mkuu wa Israeli Benjamin Netanyahu.

Akiwahutubia wanahabari katika ofisi yake, Trump aliitaja siku hiyo kuwa ya kihistoria na kwamba anaamini mataifa mengine yatafuata mkondo huo.

Mwezi uliopita, Umoja wa Falme za Kiarabu ulikubali kurejesha uhusiano wa kawaida na Israel chini ya mkataba uliosimamiwa na Marekani unaotarajiwa kutiwa saini katika sherehe itakayoandaliwa katika ikulu ya White House siku ya Jumanne, itakayoongozwa na Rais Trump anayetafuta kuchaguliwa tena kama rais katika uchaguzi wa Novemba 3.

Sherehe hiyo inatarajiwa kuhudhuriwa na Waziri Mkuu wa Israeli Benjamin Netanyahu na Waziri wa Mambo ya Nje wa Muungano wa Falme za Kiarabu Sheikh Abdullah bin Zayed al-Nahyan.

**DW**

**Ikulu ya White House nchini Marekani imesema Rais Donald Trump alitoa tangazo hilo kupitia ukurasa wake wa twitter baada ya kuzungumza kwa njia ya simu na mfalme wa Bahrain Hamad bin Isa Al Khalifa na waziri mkuu wa Israeli Benjamin Netanyahu.**



# KIWANGO CHA GABRIEL CHAMKUNA ARTETA

**LONDON, England**

MIKEL Arteta alifurahishwa na kiwango cha Gabriel Magalhães wakati akicheza mchezo wake wa kwanza kwa Arsenal huku akifunga bao moja kwenye ushindi wa 3-0 dhidi ya Fulham juzi.

Mlinzi huyo wa kati alifunga bao la pili kwa Arsenal, akiunganisha mpira wa kona wa Willian kwenye mchezo huo uliopigwa Uwanja wa Craven Cottage.

Ulikuwa mchezo wa kwanza wa ushindani kwa Gabriel tangu alipocheza kwenye ushindi wa 1-0 kwenye Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, akiichezea Lille dhidi ya Lyon, kabla ya msimu kufutwa kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Pia kulikuwa na kiwango kingine cha kuvutia kutoka kwa nyota wa zamani wa Chelsea, Willian, ambaye alimtengeneza Alexandre Lacazette aliyefunga bao la kwanza kabla ya kutoa pasi ya mwisho kwa Pierre-Emerick Aubameyang aliyefunga bao la tatu.

Kocha Arteta alimsifia zaidi Gabriel, ambaye kwenye mchezo huo alipiga pasi 107.

"Wote walicheza vizuri sana," alisema Arteta baada ya mchezo huo akiwaambia waandishi wa habari.

"Kwa upande wa Gabriel, ilikuwa changamoto kubwa kwake yeye kwa sababu hakucheza soka kwa kipindi cha miezi sita.

"Kwa uhakika kabisa alicheza kwa kiwango kizuri, ili kuthibitisha uwezo wake, nilitaka kumpa muda mchache wa kucheza kwa sababu alifanya mazoezi kwa siku chache na timu.

"Lakini alikuwa kwenye kiwango cha kuvutia zaidi tofauti na matarajio, kwa hakika ameonyesha uwezo wake."

# Messi aichezea Barca kwa mara ya kwanza

**BARCELONA, Hispania**

LIONEL Messi aliichezea kwa mara ya kwanza Barcelona tangu jaribio lake la kutaka kuondoka klabuni hapo kushindikana, akicheza kwenye mchezo wa kirafiki dhidi ya Gimnastic de Tarragona.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 33 raia wa Argentina, alituma maombi ya kutaka kuondoka Agosti mwaka huu, lakini akaamua kubaki wiki iliyopita kwa sababu hakuna klabu ambayo ingeweza kumnunua kwa kiasi cha fedha kilichopo kwenye mkataba wake.

Messi alianza katika ushindi wa 3-1 dhidi ya timu hiyo ya daraja la tatu baada ya klabu hiyo kuthibitisha atabaki kuwa nahodha wa timu. Ousmane Dembele alianza kwa kufunga bao la kwanza, huku Antoine Griezmann na Phillipe Coutinho kila mmoja akifunga kwa penalti.

Messi, mfungaji wa wakati wote wa Barcelona, aliamini kwamba kipengele cha mkataba wake bado kinafanya kazi na hivyo hivyo angeweza kuondoka akiwa huru.

Barcelona na La Liga walisisitiza kipengele hicho kimeshaisha muda wake na hivyo klabu inayotaka kumnunua lazima ilipe euro milioni 700 na Messi alirudi mazoezini baada ya kusema hawezi kuishtaki klabu hiyo mahakamani.

Barca itaanza msimu huu Jumapili ya Septemba 27 itakapokuwa kwenye dimba lake nyumbani kucheza na Villarreal.

# Rodriguez atarajia majina makubwa kutua Everton

**LONDON, England**

JAMES Rodriguez ana matumaini "majina makubwa" mengine yatatua hapo Everton wakati wakijipanga kwa ajili ya msimu imara wa 2020-21.

James alijiunga na klabu hiyo ya Ligi Kuu ya England akitokea kule Real Madrid kwa ada iliyoripotiwa kuwa pauni milioni 20 mapema mwezi huu na ana matumaini makubwa ya kupata mafanikio hapo Everton.

Mchezaji huyo alijiunga na kocha wake wa zamani, Carlo Ancelotti, ambaye alimnoa kule Madrid na Bayern Munich, wakati Everton ikiangalia kuimarika zaidi ya msimu uliopita ambapo walimaliza nafasi ya 12.

James mwenye umri wa miaka 29, ana matumaini ataimarika zaidi pale Goodison Park.

"Tunaweza kupaa kwa kiwango cha kuvutia zaidi msimu huu. Inasaidia zaidi hasa unapokutana na kocha anayekujua na mwenye uelewa," alisema James akinukuliwa na Televisheni ya Liverpool.

"Klabu imejiweka imara zaidi kwa kusajili wachezaji watatu wakati wa dirisha hili la usajili na tunaamini kwamba ndani ya miezi michache ijayo, tunaweza kupata wengine."

James ni mmoja kati ya wachezaji wanne pale Everton, pamoja na Allan, Abdoulaye Doucoure na Niels Nkounkou pia wametua hapo.






# MAGUIRE

## KUENDELEA NA UNAHODHA MAN UNITED

**MANCHESTER, England**

HARRY Maguire atabaki kuwa nahodha wa Manchester United kwa msimu huu licha ya kupatikana na hatia ya kuwatukana polisi nchini Ugiriki, kocha Ole Gunnar Solskjaer amesema.

Mahakama ya Syros ilimkuta na hati Maguire, ya kuwatukana na kuwatishia polisi, wakati akiwa kwenye mapumziko nchini humo na mwezi uliopita.


Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, ambaye alikanusha tuhuma hizo, lakini mahakama ilimhukumu baada ya kumkuta na hatia katika vurugu hizo alizozifanya katika Kisiwa cha Mykonos.

Mwanasheria wa Maguire alikata rufani ya hukumu hiyo na sasa wanasubiri kusikilizwa upya kwa kesi hiyo.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa England, alitemwa na kocha, Gareth Southgate kwenye kikosi cha Taifa kwa ajili ya mashindano ya Ligi ya Mataifa ya UEFA kutokana na kesi hiyo.

Akizungumza kabla ya mchezo wa kujipima nguvu wa kirafiki wa United dhidi ya Aston Villa juzi Jumamosi, Solskjaer alithibitisha kwamba, ataendelea kuwa nahodha.

"Bila shaka yoyote Harry ataendelea kuwa nahodha wa Manchester United," alisema akiiambia televisheni ya MUTV.




## NEYMAR ASAINI DILI JIPYA NA PUMA

**PARIS, Ufaransa**

NEYMAR amesaini dili jipya na kampuni ya vifaa vya michezo ya Puma baada ya kumaliza mkataba wake na Nike.

Nyota huyo wa kimataifa wa Brazil, hivi karibuni alitangaza kumaliza mkataba wake na kampuni ya vifaa vya michezo ya Nike kutoka nchini Marekani ambapo alikuwa amebakiza miaka miwili kumaliza mkataba huo, ambao uliripotiwa kuwa na thamani ya euro milioni 100.

Puma ilisema katika taarifa yake kwamba, mshambuliaji huyo wa Paris Saint-Germain sasa atakuwa na Puma na kuwa balozi wake ndani na nje ya uwanja.

Akizungumzia kuhusu dili hilo jipya, Neymar ambaye aliandika kwenye ukurasa wake wa twitter "mfalme amerudi", alisema maamuzi yake ilikuwa sehemu ya kutaka kupita sehemu waliyopita magwiji, Pele na Diego Maradona ambao nao walijihusisha na kampuni hiyo.

"Nimekua huku nikiangalia video ya wanasoka magwiji duniani kama vile Pele, (Johan) Cruyff, (Lothar) Matthaus, Eusebio na Maradona," aliandika Neymar.

"Hawa walikuwa wafalme wa uwanjani, wafalme wa michezo. Nataka kurudisha tena heshima waliyoiweka uwanjani.

"Walicheza chini ya Puma, na wote walitengeneza ufalme wao uwanjani."

# Simeone wa Atletico akutwa na corona



**MADRID, Hispania**

KOCHA Mkuu wa Atletico Madrid, Diego Simeone, amekutwa na vizuri vya corona, klabu hiyo ya LaLiga imethibitisha.

Kikosi chote cha Atletico na benchi la ufundi kilifanyiwa vipimo vya ugonjwa wa COVID-19 Ijumaa baada ya kurudi kutoka kwenye kambi ya kujiandaa na msimu mpya jijini Los Angeles nchini Marekani.

Na baada ya vipimo hivyo, Simeone alikutwa na virusi ingawa hana dalili yoyote ya homa, kwa sasa amejitenga kwa siku 14.

"Baada ya vipimo imebainika kocha, Diego Pablo Simeone amekutwa na maambukizi ya ugonjwa wa COVID-19," ilisema taarifa ya Atletico.

"Bahati nzuri, mwalimu wetu hajaonyesha dalili zozote za ugonjwa na sasa amejitenga nyumbani kwake.

Atletico inatarajia kucheza mchezo wa kirafiki na Cadiz kesho Jumanne kabla ya kuanza kampeni ya Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, nyumbani dhidi ya Granada, Septemba 27, mwaka huu.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# KLOPP: HUYU SALAH NI MCHEZAJI MAALUMU

●●● Ni baada ya kupiga hat-trick, asema alistahili mabao 100, na kulikuwa na penalti mbili...

**LIVERPOOL, England**

JURGEN Klopp amemsifia Mohamed Salah kama "mchezaji maalumu" baada ya nyota huyo wa Liverpool kufunga mabao matatu 'hat-trick' kwenye ushindi wa 4-3 dhidi ya Leeds United.

Kikosi hicho kinachonolewa na kocha, Marcelo Bielsa ambacho kimepanda daraja kilikutana na kipigo hicho kutoka kwa mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu ya England, kwenye mchezo uliopigwa pale katika dimba la Anfield, Jumamosi.

Hata hivyo, Liverpool ilisubiri hadi penalti ya utata ya Salah ili kuweza kuibuka na ushindi huo wa mabao 4-3.

Salah alianza kwa kufunga bao la ufunguzi kwa penalti baada ya Robin Koch kuunawa mpira, kabla ya Jack Harrison kusawazisha.

Mlinzi Virgil van Dijk aliwarudisha Liverpool mchezoni kwa kufunga la pili, kabla ya Patrick Bamford kusawazisha na Salah akafunga la tatu, na Mateusz Klich akasawazisha.

Zikiwa zimesalia dakika mbili kumalizika Salah akafunga la nne na kuwapa ushindi huo, huku Klopp akibaki kuamini kwamba mshambuliaji huyo wa Misri ni mchezaji wa aina yake.

"Kwanza nampongeza sana, lakini yeye ni mchezaji maalumu, maalumu kwa ajili ya mechi muhimu," alisema kocha huyo wa wekundu hao.

"Alistahili mabao 100, ndio kulikuwa na penalti mbili na moja ilikuwa muhimu zaidi katika dakika za majeruhi. "Ukiwa na mchezaji maalumu kwenye kikosi chako unakuwa kwenye mazingira mazuri zaidi ya kukupa ushindi wakati wowote."

## KWA UFUPI

**UNITED YAJITOSA KWA BALE**

KLABU ya Manchester United, huenda ikawasilisha ombi la kumsajili winga wa Real Madrid na Wales, Gareth Bale kama mbadala wa winga wa Borussia Dortmund na England, Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 20. ***(Sunday Express)***

**KOEMAN AMTAKA SALAH**

KOCHA mpya wa Barcelona, Ronald Koeman amemfanya mshambuliaji wa Misri Mohammed Salah kuwa ndio chaguo lake la kwanza msimu huu. ***(Sunday Express)***

**REGUILON KWENDA SEVILLA**

MLINZI wa kushoto wa Hispania, Sergio Reguilon mwenye umri wa miaka 23, angependelea kuhamia kwa mkopo katika klabu ya Sevilla badala ya Manchester United. ***(AS)***

**SPURS YAKWAMA KWA BELOTI**

OMBI la Tottenham Hotspur la kutaka kumsajili kumsajili mshambuliaji wa Italia na Torino, Andrea Beloti limekataliwa. ***(Sky Italia - in Italian)***

**UNITED YAMUWINDA BADIASHILE**

MANCHESTER United imejiandaa kutua Monaco ili kumsajili mlinzi wake, Benoit Badiashile mwenye umri wa miaka 19, kwa dau la pauni milioni 23. ***(L'Equipe, via Sunday Express)***

**CONTE KUMSAJILI ALONSO**

KOCHA wa Inter Milan, Antonio Conte anataka kumleta katika klabu hiyo beki wa kushoto wa Chelsea na Hispania, Marcos Alonso mwenye umri wa miaka 29. ***(Sky Italia, via Mail on Sunday)***

**PAULINHO AWANIWA TOTTENHAM**

KLABU ya Tottenham inajiandaa kuwasilisha ombi la kumnunua mshambuliaji wa Braga na Ureno, Paulinho mwenye umri wa miaka 27. ***(90min)***

**TOURE HAFIKIRII KUSTAAFU**

KIUNGO wa zamani wa Manchester City na Ivory Coast, Yaya Toure mwenye umri wa miaka 37, hana mpango wa kustaafu na sasa anataka kucheza katika Ligi ya Serie A. Kwa sasa ni mchezaji huru baada ya kuondoka katika klabu ya nchini China ya Qingdao Huanghai Januari. ***(Tuttomercato via Goal)***

**WEST HAM YAMUWINDA SOLLY**

KLABU ya West Ham inamnyatia winga wa Brighton na England, Solly March mwenye umri wa miaka 26. ***(90min)***

**CHOUIAR AGOMBEWA EPL**

MSHAMBULIAJI wa Dijon na Ufaransa, Mounir Chouiar mwenye umri wa miaka 21, anawaniwa na klabu za Leeds, Wolves na Arsenal. ***(France Football)***

**LEEDS KWA GALLAGHER**

KLABU ya Leeds inataka kumnunua kiungo wa kati wa Chelsea na England, Conor Gallagher mwenye umri wa miaka 20. ***(Mail on Sunday)***



HABARI MICHEZO

# KATWILA AZITISHA SIMBA NA YANGA

**Na Somoe Ng'itu, MOROGORO**

KOCHA Mkuu wa Mtibwa Sugar, Zuberi Katwila, amewataka vigogo wa soka nchini, Simba na Yanga, kujipanga kupokea matokeo ya 'kuumiza' katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu kutoka kwa timu yake.

Katwila ametoa kauli hiyo baada ya kutoka sare ya bao 1-1 dhidi ya mabingwa watetezi, Simba katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara uliochezwa juzi kwenye Uwanja wa Jamhuri mkoani hapa.

Kocha huyo aliliambia gazeti hili kuwa timu yake imesajili wachezaji wapya ambao wameingia kukiimarisha kikosi hicho na hatarajii kuona wanapata matokeo mabaya kama ilivyokuwa katika msimu uliopita.

Kiungo huyo wa zamani wa timu hiyo, alisema nyota nane aliowasajili juzi walianza katika kikosi cha kwanza na wako tayari kuipa Mtibwa taji la Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya kulikosa kwa muda mrefu.

"Nimefanya mabadiliko makubwa kwenye kikosi changu, katika mchezo wa leo (juzi), nimetumia wachezaji wapya nane ambao nimewapanga katika nafasi muhimu za wachezaji wenyeji na wamefanya vizuri, hawakuwa wageni kama tulivyotarajia, wamefanya kazi nzuri sana," alisema Katwila.

Aliongeza pointi moja waliyoipata kwa Simba ni muhimu sana katika hesabu zao na anaamini wanakoelekea watavuna ushindi na kujiweka kwenye nafasi nzuri zaidi kwenye msimamo wa ligi.

"Hii ni ligi, pointi moja ni muhimu sana, nimeona mazuri nitayaboresha na mapungufu nitayafanyia kazi kuelekea mchezo unaofuata, ndio mwanzo na kila siku wachezaji wanajifunza vitu vipya vinavyowajenga na kuwaimarisha, naweza kusema msimu huu nasi tumepania," aliongeza kocha huyo.

Alieza kila mechi kwao ni muhimu na hawataiogopa au kuidharau timu yoyote inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu kwa sababu kila moja inapambana kuwania ufalme wa nchi.

"Ningependa tena niwapongeze kwa kupata pointi hii moja, ligi ni ngumu, tutapambana kusaka ushindi, leo (juzi), tumecheza na timu kubwa na haijalishi tunacheza na Simba au Yanga, kwetu sisi kazi yetu ni moja tu, kutafuta ushindi," alisema Katwila.

Naye Msemaji wa Mtibwa Sugar, Thobias Kifaru, alitamba timu yao msimu huu 'imekuja tofauti' na itatoa vichapo kwa timu mbalimbali na kuitaja Simba imenusurika.

"Mimi msimu huu niko vizuri sana, msimu huu watatutambua, sitawaomba mtuombee dua ya kunusurika kushuka daraja kama ilivyokuwa katika dakika za mwisho msimu uliopita, waambieni wajipange," Kifaru alisema.

KIDEDEA...



Mshindi wa mita 1,500 wa mashindano ya Riadha Taifa kwa upande wa wanaume, Mbaraka James, akishangilia baada ya kushinda kwenye mbio hizo zilizofanyika Uwanja wa Mkapa jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Hitimana, Malale ni vita vya tatu leo

**Na Saada Akida**

WAKATI Kocha Mkuu wa Polisi Tanzania, Hamsini Malale, akisema wameenda Ruangwa, Lindi kutafuta alama tatu muhimu dhidi ya wenyeji wao katika mchezo utakaopigwa leo kwenye Uwanja wa Majaliwa, Kocha wa Namungo FC, Hitimana Thierry amesema mkakati wao ni kuvuna pointi zote wakiwa dimba la nyumbani.

Akizungumza na gazeti hili jana, Malale alisema kikosi chake kipo tayari kwa ajili ya mechi kuhakikisha wanapata matokeo chanya.

Alisema mechi hiyo itakuwa ya ushindani mkubwa kwa sababu hawako tayari kukubali kupoteza pointi kwa mara ya pili na wenyeji wao watakuwa wananahitaji kuweka heshima uwanja wao wa nyumbani.

"Mechi ya ushindani mkubwa, kwa upande watu, tunahitaji kupata alama muhimu, pia hatutakuwa tayari kupoteza kama ilivyokuwa mchezo wetu wa kwanza dhidi ya Azam," alisema Malale.

Naye kocha wa Namungo, Hitimana, alisema mipango yao ni kuhakikisha hawapotezi pointi katika michezo yao mitano ya mwanzo na kuandaa wachezaji wake kupambana kutafuta alama tatu katika mechi zao zote za ligi hiyo hasa wanapocheza uwanja wa nyumbani.

Alisema wameanza vizuri msimu huu wa 2020/21 kwa kupata alama tatu katika mechi yao dhidi ya Coastal Union ambayo msimu uliopita alipata wakati mgumu mbele ya timu hiyo kwa kupoteza alama tatu katika uwanja wao.

"Coastal ipo vizuri sana, kwani sisi tulicheza kwa malengo ya kuhakikisha tunalinda heshima ya nyumbani kuhakikisha tunabakiza pointi tatu, hilo tumefanikiwa na sasa nguvu na akili zetu tunazielekeza katika mchezo wetu ujao dhidi ya Polisi Tanzania, kwamba hakuna timu itakayoondoka na alama tatu katika uwanja wetu wa nyumbani," alisema Hitimana.

## Dube aifungua mdomo Azam

**Na Saada Akida**

KOCHA Msaidizi wa Azam FC, Vivier Bahati, amesema kasi ya mshambuliaji wao, Mzimbabwe Prince Dube, inawapa matumaini ya kumaliza tatizo lao la msimu uliopita kwenye safu ya ushambuliaji, ambayo ilishindwa kupata idadi kubwa ya mabao.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Vivier alisema ana imani usajili uliofanywa msimu huu umetatua tatizo la msimu uliopita hasa katika safu ya ushambuliaji kwa kuinasa saini ya Dube.

Alisema nyota huyo kwa kushirikiana na wenzake atakuwa msaada mkubwa katika kikosi chao hasa katika kupata idadi kubwa ya mabao.

"Ana uwezo mzuri pia umri wake ni mdogo, hapa anatumika kama winga, ila nafasi yake ni mshambuliaji wa kati, kwa kasi yake tuna matumaini makubwa msimu huu kupata idadi nzuri ya mabao na kushinda," alisema Vivier.

Alisema msimu huu wamejipanga vizuri kuhakikisha wanapata alama muhimu katika kila mechi nyumbani na ugenini.

Kocha alisema kikosi hicho kimeingia kambini jana kuendelea na programu ya mechi yao ijayo dhidi ya Mbeya City watakayocheza ugenini katika Uwanja wa Sokoine Jumapili ijayo.

Katika mechi iliyopita, Dube alicheka na nyavu mara mbili wakati wakishinda 2-0 dhidi ya Coastal Union kwenye mechi iliyopigwa Uwanja wa Azam Complex, Chamazi jijini Dar es Salaam.

## Kocha JKT akubali muziki Dodoma Jiji

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa JKT Tanzania, Mohamed Bares, amesema kipigo cha mabao 2-1 walichokipata nyumbani dhidi ya Dodoma Jiji FC kilitokana na kuzidiwa, ikiwamo kufanya makosa kadhaa ambayo wapinzani wao walifanikiwa kuyatumia.

Bares amesema mechi ilikuwa nzuri na anawapongeza Dodoma Jiji kwa mchezo mzuri na wameshinda kihalali na kwa ushindi huo wala hana tatizo nao.

"Niwapongeze walicheza vizuri, na sisi pia tumecheza vizuri, lakini wenzetu walituzidi kwa kuwa yale makosa ambayo tumeyafanya wameweza kuyatumia," alisema Bares.

Alisema kuwa baada ya mechi hiyo ameona baadhi ya makosa na mapungufu kwenye kikosi chake ambayo anaenda kuyafanyia kazi.

**"Mpira ni mchezo am bao hautabiriki, leo tu mecheza kadri ya uwezo wetu, lakini wenzetu wametuzidi kwa ku tumia nafasi, yame pita na sasa tunasonga mbele," alisema kocha huyo baada ya timu yake kukubali kipigo cha ma bao 2-0 katika Uwanja wa Jamhuri jijini Dodo ma juzi.**

# Michezo

Jumatatu Septemba 14, 2020

Nipashe




KLOPP: HUYU SALAH NI MCHEZAJI MAALUMU

HABARI UK 22

## SAMATTA SASA AANZA KUKIMBIZWA ASTON VILLA

**Na Mwandishi Wetu**

MSHAMBULIAJI wa kimataifa wa Tanzania, Mbwana Samatta, ameanza kupata changamoto ya kuwania namba katika kikosi cha kwanza cha Aston Villa huku usajili mpya katika nafasi hiyo, Ollie Watkins akianza kumkimbiza kwa kufunga bao katika mechi yake ya kwanza kuichezea timu hiyo.

Samatta aliingia akitokea benchi dakika ya 66, kuchukua nafasi ya mfungaji wa bao pekee, Watkins, wakati wakishinda 1-0 dhidi ya Manchester United kwenye mechi ya kirafiki iliyopigwa Uwanja wa Villa Park juzi.

**Watkins aliyesajiliwa majira haya ya joto akitokea Brentford kwa ada iliyoweka rekodi Aston Villa, kiasi cha pauni milioni 28 ambazo zinaweza kuongezeka na kufikia pauni milioni 33, alifunga bao hilo pekee katika dakika ya 16.**

Kiungo Mmisri Mahmoud Ahmed Ibrahim maarufu Trezeguet, ndiye aliyemtengenezea bao hilo Watkins, ambaye kwa kiwango alichoonyesha kinaonyesha anakwenda kuwa tishio kwa Samatta katika kuwania namba kikosini hapo.

Wakati Ligi Kuu England ilianza rasmi juzi, Jumamosi, timu hizo zilikubaliana kucheza mechi ya kirafiki kutokana na mechi zao za ufunguzi za ligi hiyo kuahirishwa.

Manchester United ilikuwa ianze na Burnley kwenye Uwanja wa Turf Moor na Aston Villa walitakiwa kuwafuata Manchester City kwenye dimba la Etihad, lakini mechi hizo ziliahirishwa ili kuzipa nafasi zaidi timu hizo za Jiji la Manchester kujiandaa kutokana na kushiriki michuano ya klabu barani Ulaya hadi hatua za mwishoni.




**KAMA UPINDE...**

Mshambuliaji wa Arsenal, Pierre-Emerick Aubameyang, akiachia shuti lililosafiri mithili ya upinde wa mvua na kujaa nyavuni wakati akiiandikia timu yake bao la tatu na kuiwezesha kushinda 3-0 ugenini dhidi ya Fulham kwenye mechi ya ufunguzi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Craven Cottage jijini London juzi. **PICHA: MTANDAO**

# SVEN: SAFARI UBINGWA SIMBA TUNAIANZA J'PILI

●●●Ashukuru kuondoka na pointi Mtibwa, asema Biashara United wasubiri...

**Na Somoe Ng'itu, MOROGORO**

BAADA ya timu yake kuambulia sare ya bao 1-1 dhidi ya Mtibwa Sugar juzi, Kocha Mkuu wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, Mbelgiji Sven Vandenbroeck, amesema matokeo hayo si mabaya, ila safari ya kuanza vema kutetea ubingwa wa ligi hiyo wataianza rasmi katika mechi ijayo dhidi ya Biashara United itakayopigwa Uwanja wa Mkapa Jumapili ijayo.

Akizungumza na Nipashe mjini hapa, Sven, alisema mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Jamhuri, ilikuwa na ushindani na yenye changamoto kuanzia dakika ya kwanza hadi ya mwisho na hali hiyo ilisababishwa na kila upande kuingia uwanjani ukiwa na malengo tofauti.

Sven aliwapongeza wachezaji wake kwa kutokata tamaa katika mchezo huo, ambapo Mtibwa Sugar wakijipanga kutumia nguvu zaidi kila walipopoteza mpira.

"Ilikuwa ni mechi ngumu, yenye ushindani na ufundi, timu zote mbili zimebadilika ukilinganisha na zilivyokuwa msimu uliopita, lakini kikubwa tulifanikiwa kuondoka na pointi moja, si matokeo mabaya ingawa hayakuwa malengo yetu kupata sare," alisema Sven.

Aliongeza kikosi kinarejea jijini Dar es Salaam kuendelea kujifua kwa ajili ya mchezo unaofuata dhidi ya Biashara United ambao anaamini kazi ya kuwapa furaha itaanzia hapo.

"Mechi za kwanza huwa ngumu na zisizotabirika, ila safari ya kutetea ubingwa iko pale pale na tutaianza vema katika mechi yetu inayofuata, kwa sasa ni mapema kusema lolote maana ndio kwanza imeanza, huku pia tukijipanga na mashindano ya kimataifa," alisema kocha huyo raia wa Ubelgiji.

Aliongeza anafurahishwa na kiwango cha kila mchezaji katika kikosi chake kwa sababu wote malengo yao ni kuisaidia timu ifanye vizuri katika Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano yote watakayoshiriki.

Meneja wa Simba, Patrick Rweyemamu, alisema Mtibwa Sugar ni moja ya timu zenye wachezaji wazuri na matokeo waliyopata katika mchezo wa juzi si mabaya.

"Kila timu ilijipanga na iliingia uwanjani ikiwa na mipango yake, kama wangetulia wangepata ushindi na sisi pia tulipata nafasi kama tatu za wazi, lakini kipa wao alikuwa imara na alisimama nafasi sahihi langoni mwake," alisema meneja huyo.

Alimtaja mchezaji ambaye ni majeruhi kuwa bado ni Charles Ilanfya, huku nyota wengine wageni ambao hawakupangwa ilitokana na uamuzi wa kocha na si sababu nyingine.

Haji Manara, Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba alisema: "Asante Mungu, kupata pointi nne ugenini, si jambo dogo, vijana wanarejea Dar es Salaam kwa ajili ya kupambana kupata ushindi katika mechi zinazofuata, hii ni ligi, hakuna mechi ndogo wala kubwa".

Simba ambao baadaye mwaka huu wataiwakilisha Tanzania Bara katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika ina pointi nne katika nafasi ya nne kwenye msimamo wa ligi hiyo, wakati vinara kabla ya mechi ya jana usiku kati ya Yanga dhidi ya Mbeya City ni KMC FC na Dodoma Jiji FC ambao kila moja ina pointi sita.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >